




**74** wafa wivu wa mapenzi, kujinyonga

UKURASA 3



POGBA YUKO NJIA MOJA

UKURASA 22

Nipashe
Ijumaa Februari 18, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580860
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Walichoteta Samia na Lissu ughaibuni

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo ya Ubelgiji, Luxembourg, Afrika, Caribbean na Pacific (CBL-ACP), Brussels nchini Ubelgiji jana. **PICHA: IKULU**

## TMA yatoa tahadhari mvua kubwa msimu masika

UKURASA 3



IGP Simon Sirro.

## Wabunge wataka chombo huru kuwachunguza polisi

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA SC GARI LIMEWAKA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na wakurugenzi wa bodi alipotembelea kwa mara ya kwanza ofisi zao, Mazizini jijini Zanzibar. **Habari UK. 4. PICHA: IKULU**

# Walichoteta Samia na Lissu ughaibuni

**Na Romana Mallya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ameweka wazi walichozungumza na Rais Samia Suluhu Hassan juzi ughaibuni Brussels, Ubelgiji.

Lissu ambaye kitaaluma ni mwanasheria, amesema kuwa katika mkutano wao huo, waliteta mambo sita na Mkuu wa Nchi huyo, ikiwamo hatima ya Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, anayekabiliwa na kesi ya ugaidi.

Muda mfupi baada ya Mkurugenzi wa Mawasiliano Ofisi ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, kutoa taarifa kuhusu Rais Samia kukutana na Lissu kwa mazungumzo Ubelgiji juzi, Lissu alizungumza kwa njia ya mtandao kufafanua baadhi ya mambo waliyoteta.

Lissu alisema ajenda kubwa ilikuwa ni hali ya kisiasa nchini na kumpatia Rais Samia ujumbe wa CHADEMA kuhusu masuala mbalimbali.

"Katika masuala ambayo nimemweleza Mheshimwa Rais, moja, nimezungumza naye kwa kirefu kuhusiana na kesi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Mbowe.

"Nimemwambia Rais wetu, hiyo kesi haiisaidii nchi yetu, haisaidii serikali yake, haikisaidii chama chake, haikisaidii chama chetu. Inamuumiza mwenyekiti wetu na familia yake, inawaumiza walinzi wake na familia zao na inazidi kutugawa Watanzania," alidai.

Lissu alisema alimwambia Rais Samia kuwa afanye analoweza kwa mamlaka yake kuhakikisha kesi hiyo inaondolewa mahakamani.

"Hakuna sababu yoyote ya kuendelea na kesi ambayo kila mtu anaona na ushahidi unaonyesha mahakamani ni mambo ya kuungaunga tu. Rais ameahidi kwamba atalishughulikia, Lissu alidai.

Lissu alitaja ajenda ya pili kuwa ni hali ya vyama vya siasa hasa vya upinzani ambavyo vinakumbana na vikwazo katika kufanya shughuli za kisiasa kutokana na kuwapo kwa vizuizi vilivyo nje ya sheria.

"Nimemwambia Mheshimiwa Rais akafute hili zuio la vyama vya siasa vya upinzani kufanya mikutano ya hadhara pamoja na maandamano kama sheria za Tanzania zinavyoruhusu," alisema.

Lissu alisema alimweleza Rais kuwa ni suala la kuheshimu sheria za nchi kama zilivyo, akifafamua: "Sheria kama zilivyo zinasema vyama vya siasa vina haki ya kufanya mikutano na maandamano, vina haki ya kupatiwa ulinzi na Jeshi la Polisi pamoja na vyombo vingine vya usalama vinapofanya mikutano na maandamano hayo.

"Tumezungumza kwa kirefu, na Mheshimiwa Rais amesema vilevile hilo analishughulikia. Kwa hiyo, tumeachia hapo. Jambo la tatu linahusu suala la katiba mpya na mfumo mpya na wa kidemokrasia wa uchaguzi kwa ajili ya nchi yetu.

"Nimemwambia Mheshimiwa Rais kwamba ana fursa ya kipekee na ya kihistoria ya kuipatia nchi yetu katiba mpya na ya kidemokrasia, ana fursa ya kipekee na ya kihistoria ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata mfumo mpya na wa kidemokrasia wa uchaguzi utakaohakikisha tunakuwa na tume huru ya uchaguzi.

"Utakaohakikisha sheria zetu za uchaguzi ni sheria za kidemokrasia zinazohakikisha haki sawa kwa wote wanaoshiriki uchaguzi, kuhakikisha uchaguzi ujao unakuwa huru, wa haki na unaokubalika," alisema.

Lissu alisema wamezungumza na Rais kwamba mjadala wa katiba mpya utakuwa mrefu lakini ni muhimu wajadili suala hilo.

Alisema ajenda ya nne ilimhusu yeye (Lissu) na wenzake ambao wamelazimika kuikimbia nchi kutokana na kile alichokiita vitisho dhidi ya maisha yao.

Lissu alisema kwa vile Rais ana mamlaka ya kuhakikisha anapata haki alizonyimwa baada ya kushambuliwa Septemba 2017, ikiwamo haki ya kupatiwa matibabu kwa mujibu wa sheria, amemwomba alishughulikie suala hilo, akidai kuwa Mkuu wa Nchi amelichukua.

"Nimezungumza na Rais kuhusiana na mazingira yote yanayohusu kuondolewa kwangu bungeni mwezi Juni, 2019 na kutokulipwa kiinua mgongo kinyume cha sheria husika, nimemweleza mimi ni mbunge pekee sikulipwa mafao yangu, ameahidi kulishughulikia," alisema.

Pia alisema amemweleza Rais kuwa anahitaji kurudi Tanzania kama alivyotangaza awali na kumwomba atoe kauli ya kumkaribisha, akidai Mkuu wa Nchi pia ameahidi kulifanyia kazi.

Lissu pia alisema amezungumza hayo kwa niaba ya Godbless Lema na Ezekiel Wenje ambao walikwenda Canada baada ya kuikimbia nchi kwa madai ya kuwapo vitisho dhidi ya usalama wao.

Alisema ajenda ya tano ni uhalali wa wabunge 19 walioibua mvutano kati ya uongozi wa Bunge na CHADEMA, chama hicho cha siasa kikitangaza kuwafuta uanachama, hivyo kukosa sifa mojawapo ya kuitwa wabunge.

Lissu alisema amemweleza Rais kuwa CHADEMA haina wabunge bungeni na kumwomba Rais alishughulikie kwa sababu Watanzania hao 19 kuendelea kulipwa posho za ubunge ni ufujaji wa fedha za umma.

"Ajenda ya mwisho katika mkutano wetu ilikuwa ajenda ya ujumla, nimemwambia Mheshimiwa Rais atuongoze, yeye ni Rais wetu sote. Kwa sababu ni Rais, ana jukumu la kipekee la kutuongoza na kusaidia kuiponya nchi yetu," Lissu alihitimisha.

**WADAU**

Akizungumzia mkutano huo, Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema: "Hatimaye hekima imetawala na mlango wa mazungumzo umefunguka.

"Sisi ACT-Wazalendo tokea awali tulisisitiza kwamba mazungumzo ndiyo njia sahihi ya kupata ufumbuzi wa tofauti zetu za kisiasa na kuleta mabadiliko. Hatua ya Rais kukubali kuonana na Lissu ni ya kupongezwa sana."

Wakili Fatma Karume alisema "I am proud of you, SSH (Samia Suluhu Hassan). Lissu proud of you too. Tunahitaji demokrasia. Hakuna kinacho mwanzo kisichoisha!"

Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) pia kimempongeza Rais Samia kwa kukubali ombi la Lissu kukutana naye kwa mazungumzo Ubelgiji, kikisisitiza kuwa mkutano huo ni muhimu katika kujenga maridhiano ya kitaifa nchini na kuwezesha kufanyika kwa siasa zenye maslahi kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Bernadetha Kafuko, katika taarifa yake jana, alisema mkutano huo kati ya Rais Samia na Lissu utarahisisha kazi za kituo kama jukwaa muhimu la majadiliano ya kisiasa nchi katika kuchochea matokeo chanya ya kuweka uwanja sawa wa ushindani wa kisiasa.

## Wabunge wataka chombo huru kuwachunguza polisi

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BAADHI ya wabunge wametaka kufumuliwa kwa muundo wa Jeshi la Polisi ili kuunda chombo huru cha kusimamia nidhamu ya askari polisi nchini na kuchunguza matukio ya uvunjifu wa haki za binadamu dhidi ya raia.

Wabunge hao zaidi ya 20 ambao ni vinara wa kutetea haki za binadamu, waliyasema hayo jana wakati wa semina kwa wawakilishi hao wa wananchi iliyoandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Mbunge wa Mlalo, Rashid Shangazi, alisema kuna mambo mengi ndani ya Jeshi la Polisi ambayo yanalazimu kufumua muundo mzima, ili kutoa baadhi ya vitengo ndani yake na kuondoa au kupunguza malalamiko na vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu.

"Kuna nchi tayari zimetenganisha vitengo vya upelelezi na uendesha mashtaka, kuna makosa hayaendi polisi aliyetendwa anaanzia kwenye kitengo husika. Mfano, matukio ya ubakaji, kwetu tuna dawati la jinsia, lakini linachukuliwa kama sehemu ya adhabu mtu akiwekwa humo.

"Mapendekezo ya kuunda tume ya kijaji ni mazuri, lakini lazima tujiulize Jeshi la Polisi tulilonalo leo, linaendana na karne ya 21? Kuna ukuaji wa teknolojia, wao bado wamebaki na mbinu zile zile, maarifa yale yale katika utendaji kazi, ndiyo maana matukio ya watu kutendwa ubaya yanaongezeka," alisema.

Mbunge wa Chakechake, Ramadhani Suleiman Ramadhani, alisema ni muhimu kuunda chombo huru cha kushughulikia nidhamu ya polisi na kuchunguza mambo mengi yanayolalamikiwa na raia.

Mbunge huyo alisema kwa Tanzania Bara kuna tofauti na ndiyo maana wanapendekeza kuundwa kwa chombo maalumu kitakachoanzishwa na katiba.

"Siyo muda wa kusubiri hadi mabadiliko ya jumla ya katiba, tunaweza kuleta mabadiliko ya baadhi ya ibara kwa kuongeza chombo huru kitakachosema muundo wake. Mwenyekiti atakayefanya kazi bila kuingiliwa na mamlaka nyingine, wapeleleze na kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya matendo ya baadhi ya polisi," alishauri.

Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba, alisema kuwapo kwa chombo huru hakutakuwa jambo la kwanza kwa kuwa nchi nyingi duniani zimeshatenganisha na hata Zanzibar imeshafanya hivyo miaka mingi.

"Ipo haja kuvunja mamlaka ya Jeshi la Polisi kwa kuwa huwezi kukamata, kupeleleza, unapeleka kesi mahakamani katika msingi wa kutenda haki, hakuna haki itatendeka kwa mazingira hayo," alionya.

"LHRC wamefungua mjadala, sasa ni wakati wa kila mmoja kushiriki muundo wa chombo huru uweje, nani awe kwenye idara gani, watu gani wahusike kwenye upelelezi. Tume itakayoundwa kuchunguza watu kuteswa kufia kwenye mikono ya polisi iweje," alisema.

Salome aliweka wazi kuwa anajipanga kupeleka hoja binafsi bungeni kushinikiza serikali kupeleka muswada wa mabadiliko ya sheria iliyounda Jeshi la Polisi ili kutenganisha majukumu kwa lengo la kuwapa wananchi haki zao za msingi.

Mbunge wa Biharamulo Magharibi, Ezra Chiwelesa, alisema hakuna namna raia anaweza kulishtaki Jeshi la Polisi na kushinda na kuna matukio mengi ya watu kuteswa ambayo hayajaripotiwa.

Mbunge wa Viti Maalum, Ng'wasi Kamani, alisema sheria imempa nguvu Waziri wa Katiba na Sheria kuunda mahakama ndogo yenye hakimu, daktari na watu wengine kuchunguza tukio la kifo lakini imezungumzia kifo pekee na siyo manyanyaso na matukio mengine ambayo ni mabaya kwa wananchi.

Awali, Maofisa Uchechemuzi wa LHRC, Raymond Kanegele na Willium Maduhu, walisema LHRC inapendekeza kuundwa Tume ya Kushughulika na Vitendo vya Utovu wa Nidhamu na Mauaji ya Wananchi wakiwa chini ya ulinzi.

Walisema kiwe na Mwenyekiti wa chombo hicho ambaye ni Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani, kuwe na Katibu Mkuu ambao watateuliwa na Rais.

Pia, wajumbe 10 kutoka Mahakama, DPP, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Umma na Utawala Bora, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Tume ya Utumishi ya Wizara ya Mambo ya Ndani na wateuliwe kutoka pande zote za Muungano.

HABARI KITAIFA

# TMA yatoa tahadhari mvua kubwa masika

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetoa tahadhari ya kuwapo mvua kubwa za wastani mpaka juu ya wastani katika kipindi cha masika (Machi-Mei) kwa mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka.

Katika utabiri huo uliotolewa jana na Mkurugenzi wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, mikoa yote inayopata mvua hizo inatarajiwa kuwa na mvua kubwa na hivyo kutoa tahadhari kwa sekta mbalimbali kuchukua hatua kukabiliana na athari zinazoweza kutokea kutokana na uwapo wa mvua hiyo.

"Mifumo ya hali ya hewa inaonyesha kuwapo kwa mvua kubwa katika msimu huu wa masika na zitaanza kunyesha wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Februari na kumalizika mwezi Mei," alisema.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Kanda ya Ziwa (Kagera, Mwanza, Geita, Mara na Shinyanga), Tanga, Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya kaskazini mwa mikoa ya Morogoro, Pwani na visiwa vya Mafia Zanzibar.

Alisema mvua inatarajiwa kuwa ya wastani mpaka juu ya wastani ikitarajiwa kuwa na athari mbalimbali.

"Kuna athari za kisekta zinaweza kutokea kutokana na mvua hizi tunazozitarajia. TMA kwa kushirikiana na wataalamu wa sekta husika katika kikao cha wadau wa hali ya hewa kilichofanyika Februari 11, mwaka huu tumeshauri kupanga shughuli kwa kuzingatia taarifa hizi za utabiri tunazozitoa," alisema.

Aliongeza kuwa mvua hio inaweza kuleta madhara kwenye sekta ya kilimo, miundombinu na usafirishaji ambapo uharibifu unaweza kutokea kwenye maeneo hayo.

Hata hivyo, alisema mvua hiyo inaweza kuleta faida kwenye sekta ya nishati kwa kuongezeka kina cha maji kwenye mabwawa lakini pia kwa wakulima watakaolima mazao yanaostahimili mvua kubwa.

Alitahadharisha kuwa baadhi ya maeneo yanaweza yakakumbwa na mafuriko yatakayotokana na mvua hiyo.

"Sekta ya madini wachimbaji wanatakiwa kuchukua tahadhari kutokana na mvua hiyo ambayo inaweza ikasababisha maporomoko ya udongo kwenye machimbo.

"Kiujumla, tunashauri wananchi kufuatilia ushauri na maagizo yatakayotolewa na mamlaka husika, TMA tutaendelea kufuatilia hali ya hewa na kutoa taarifa sahihi kwa wananchi kupitia vyombo vya habari," alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera ambao unatarajiwa kuwa na mvua kubwa, Profesa Faustine Kamuzora, alisema wataanza kujipanga kukabiliana na athari zozote zinazoweza kutokea.

Alisema kuwa watachukua tahadhari zote kutokana na taarifa ya TMA ili kuhakikisha mkoa huo unakuwa salama na kufaidika na mvua inayotarajiwa.

Katika utabiri wa mvua kipindi cha vuli, TMA ilitabiri kuwapo kwa uhaba wa mvua, maeneo mengi nchini yakikabiliwa na ukame uliosababisha athari nyingi ikiwamo vifo vya mifugo kutokana na ukosefu wa malisho.

# 74 wafa wivu wa mapenzi, wizi, kujinyonga miezi 8

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WATU 74 wamefariki dunia Mkoa wa Geita kwa kujinyonga, wivu wa mapenzi na wizi kwa miezi minane kuanzia Juni mwaka 2021 hadi Januari mwaka huu.

Hayo yalibainishwa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Henry Mwaibambe, alipozungumza na viongozi wa dini katika Halmashauri ya Mji wa Geita.

Mwaibambe, alisema watu hao walikufa katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo, na kwamba kuanzia Agosti mwaka 2021 hadi Januari mwaka huu, watu 46 walifariki dunia kwa sababu mbalimbali, kati yao wawili walikufa kwa imani za kishirikina, 10 kwa wivu wa mapenzi, wanane walikufa kwa ugomvi wa kawaida, watatu kwa uhalifu na 23 kwa wizi.

Alisema kati ya Juni mwaka 2021 hadi Januari mwaka huu, watu 28 walikufa kwa kujinyonga katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Geita, hivyo kusababisha taharuki kwa wananchi wa mkoa huo.

Aliwataja waliokufa kwa kujinyonga ni Rebeca Benjamin (17), mkazi wa Kijiji Msalala Wilaya ya Nyangh'wale; Sunzu Kagiye (51), mkazi wa Kijiji cha Ilamba Wilaya ya Mbogwe; Abdallah Kubigwa (35), mkazi wa Kijiji cha Msasa Wilaya ya Bukombe; Tego Luchagula (37), mkazi wa Kijiji cha Mwingiro Wilaya ya Nyang'wale, Sophia Charles (23), mkazi wa Mseto Wilaya ya Geita na Mariam Warioba (68), mkazi wa Nyarugusu Wilaya ya Geita.

Kamanda Mwaibale aliwataja wengine ni Manumbu Ngasa (38), mkazi wa Kitongoji cha Muungano Wilaya ya Bukombe; Sheria Misungwi (47), mkazi wa Kijiji cha Nyangomango Wilaya ya Chato na Baraka Jona (20), mkazi wa Nyamahuni Wilaya ya Geita, Khadija Ryoba (27) mkazi wa Mlimani Wilaya ya Chato.

Wengine ni Saada Ndengea (14), mkazi wa Kijiji cha Bunengezi Wilaya ya Geita ambaye ni mwanafunzi wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Shinamwenda; Igeye Wiromi (90), mkazi wa Kijiji cha Busalala Wilaya ya Chato; Juma Isambula (48), mkazi wa Kijiji cha Nyamikonze Wilaya ya Nyangwale; Japhet Hamisi (26), mkazi wa Kijiji cha Saragulwa Wilaya ya Geita; Ramadhani Kulwa (30), mkazi wa Nyankumbu Wilaya ya Geita; Makacha Petro (47), mkazi wa Kijiji cha Nyamasenye Wilaya ya Chato; Dunia Musukuma (50), mkazi wa Nyankumbu Wilaya ya Geita na Bahati Ndegeya (36), mkazi wa Nyarugusu Wilaya ya Geita.

Wamo pia John Maos (27), mkazi wa Kijiji cha Luhala Wilaya ya Mbogwe; Emmanuel Sadoke (43) mkazi wa Ivuma Wilaya ya Mbogwe; Rajabu Abdalla (32), mkazi wa Kijiji cha Chanika Wilaya ya Geita, Majaliwa Njanjaruka (35), mkazi wa Kijiji cha Bugurura Wilaya ya Geita; Hidia Myeye (58), mkazi wa Kijiji cha Buseresere Wilaya ya Geita; Paulo Isack (32), mkazi wa Chibingo Wilaya ya Geita; Ndede Misonado (78), mkazi wa Kijiji cha Mwambasabi Wilaya ya Geita; Mustapha Abduli (32), mkazi wa Mwambasabi Wilaya ya Geita; Elizabeth Joseph (40), mkazi wa Bugayambelele Wilaya ya Geita; mtu asiyefahamika jina (25), aliyeokotwa katika Kijiji cha Isenyi Wilaya ya Geita na Musa Emmanueli (27), mkazi wa Katoro Wilaya ya Geita.

Kamanda Mwaibambe aliwataka viongozi wa dini kuhakikisha wanawaeleza waumini wao kuhusiana na matukio hayo na kuwahubiria maadili mema ili kukomesha matukio hayo ya kujinyonga na uhalifu katika Mkoa wa Geita.


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

### KUHUSU MABORESHO YA MFUMO WA UKUSANYAJI KODI UNAOTUMIKA KUTOA RISITI ZA KIELEKTRONIKI

**Dar es Salaam, 18 Februari, 2022:**
Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha walipakodi wote wanaotumia mashine za kutolea risiti za kielekitroniki (EFD) kuwa, wanatakiwa kufanya maboresho ya mashine zao ili kuendana na matakwa ya mfumo wa kutoa risiti za kielekitroniki zenye **"QR Code"** zinazohakikiwa moja kwa moja na mfumo.

Hivyo, Mlipakodi anaombwa kufika kwa wakala wa mashine za EFD ili kufanya maboresho kwenye mashine kuendana na itifaki mpya ya mawasiliano ijulikanayo kama **Protocol 2.1** inayoendana sambamba na maboresho ya mfumo wa EFDMS ambao uhakiki moja kwa moja risiti na ankara mara zinapotoka kwenye mashine ya kielektroniki ya kutolea risiti.

Hili ni kumbushio la mwisho, itakumbukwa kwamba tarehe **7 Desemba 2020 na tarehe 20 Januari, 2022** Mamlaka ilitoa Taarifa kwa Umma kupitia vyombo vya habari, hususani magazeti, kuhusu maboresho haya sambamba na hitaji la kuboresha mashine za EFD ndani ya kipindi cha siku thelathini kuanzia tarehe ya tangazo lile. Mamlaka pia ilitoa nyongeza ya kipindi cha siku 30 kwa walipakodi wenye mashine ya EFD ambao hawakukamilisha maboresho au kununua mashine mpya zinazoendana na maboresho ya mfumo.

Baada ya kipindi kilichotolewa awali kupita, Mamlaka imefanya tathmini na kufuatilia utekelezaji wa agizo hilo na kubaini kuwa bado kumekuwepo na baadhi ya Wafanyabiashara ambao bado hawajatekeleza agizo la kuboresha mashine zao za EFD kuendana na itifaki hiyo mpya ya mawasiliano ya Protocol 2.1.

Kwa tangazo hili, Mamlaka inatoa agizo kuwa tarehe 28 Februari 2022 ndiyo siku ya mwisho kwa wafanyabiashara wote ambao bado hawajafanya maboresho katika mashine zao wafanye hivyo ndani ya kipindi hiki. Baada ya hapo Mamlaka itachukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuzifungia mashine zote za EFD ambazo zitakuwa bado hazijafanyiwa maboresho hayo.

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Imetolewa na;**
**MKURUGENZI WA ELIMU NA HUDUMA KWA MLIPAKODI**

216710802

# Tril. 1.29/- zaongezwa kwenye bajeti

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SERIKALI imewasilisha bungeni nyongeza ya bajeti ya Sh. trilioni 1.29 na kufanya jumla ya bajeti kuu Sh. trilioni 37.98 kutoka makadirio ya Sh. trilioni 36.68.

Akiwasilisha bungeni jana Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, alisema nyongeza hiyo imelazimika kuletwa bungeni kulingana na makubaliano na Shirika la Fedha Duniani (IMF), fedha zilizopatikana zitatumika ndani ya Mwaka wa Fedha 2021/22, na hazikuwa sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Alisema kufuatia mlipuko wa UVIKO-19, serikali iliandaa Mpango Mahususi wa Kukabiliana na Athari za Kijamii na Kiuchumi za UVIKO-19 (Tanzania COVID-19, uliozinduliwa Oktoba 10, mwaka jana, wenye lengo la kuleta mapinduzi makubwa katika uchumi na maendeleo ya wananchi kwa haraka zaidi.

"Mkopo usio na riba IMF wenye thamani ya Sh. bilioni 1,310.65 (Dola za Marekani milioni 567.3) kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19 katika sekta za kiuchumi na kijamii. Kati ya kiasi hicho cha fedha, shilingi bilioni 1,079.6 ni kwa ajili ya Tanzania Bara na Dola za Marekani milioni 100( sawa na Sh. bilioni 231.0) ni kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo sehemu kubwa ya uchumi wake uliathiriwa na UVIKO-19," alisema.

"Kufuatia upatikanaji wa fedha hizo ambazo hazikuwa sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, serikali inawajibika kuwasilisha bungeni mapendekezo ya kuomba ridhaa ya Bunge kutumia fedha za mkopo huo," alisema na kuongeza:

"Kwa vile matumizi ya fedha hizi yalikuwa ya haraka kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19 na matumizi hayo yanatakiwa kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha, serikali ilifanya hatua za awali za kuishirikisha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti mwezi Oktoba 2021 na Bunge la mwezi Novemba 2021 kwa lengo la kupata uelewa wa pamoja na kuruhusu kuendelea na matumizi hayo, huku ikijipanga kuomba ridhaa ya Bunge ya matumizi ya fedha hizo kuwa sehemu ya bajeti ya mwaka 2021/22."

Mwigulu alisema wanaomba ridhaa hiyo kulingana na matakwa ya Sheria ya Bajeti sura 439 Kifungu cha 43.

Waziri huyo alisema fedha hizo zilianza kutumika mwishoni mwa mwaka 2021 na mafanikio yameonekana kama kupunguza msongamano wa wanafunzi kwa kujenga jumla ya madarasa 15,000 katika halmashauri zote 184 nchini.

Alisema serikali pia ilifanya tathmini ya nusu mwaka ya utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/22 na kubaini utekelezaji wa bajeti kwa mwaka mzima wa 2021/22 utakuwa na nakisi ya Sh. bilioni 704.9.




Waombolezaji wakiaga mwili wa aliyekuwa Mkurugenzi wa Diplomasia ya Uchumi Wizara ya Mambo ya Nje, Edwin Rutageruka, katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwinyi atumbua kamishna mkuu ZRB

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametengua uteuzi wa Kamishna Mkuu wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), Salum Yussuf Ali, ili kupisha uchunguzi wa kina wa upotevu wa fedha za makusanyo ya mapato.

Dk. Mwinyi amefikia uamuzi huo akiwa katika ofisi za ZRB, Mazizini Zanzibar alipopata fursa ya kuzungumza na uongozi wa bodi hiyo, Bodi ya Wakurugenzi ya ZRB pamoja na uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA),

Taarifa maalum iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, ilisema utenguzi wa kiongozi huyo ulifanyika jana.

Pia Dk. Mwinyi akiwa katika ofizi za ZRB, aliiagiza taasisi hizo kumsimamisha kazi na kupisha ukaguzi wa kina wa maelekezo ya Mkurugenzi wa Usajili, Ukaguzi na Upelelezi wa Walipakodi, Hashim Kombo Haji, kupisha ukaguzi wa kina wa maelekezo yake ya kuondoa taarifa za ukaguzi ambazo hatimaye hazikupelekwa kwenye bodi.

Sambamba na hayo, aliiagiza ZAECA kufanya uchunguzi kwa kushirikiana na watendaji waliofanya uchunguzi kwa kushirikiana na vikosi vyote vya ulinzi na usalama watakavyovihitaji ili kujua fedha hizo zimekwenda wapi.

Alisisitiza haja ya taarifa zote za kitengo cha uchunguzi kufanyiwa uchunguzi na kufuatiliwa ili kujua ripoti zilizotolewa na kitengo hicho hatima yake ni kitu gani.

Rais Mwinyi pia alitaka uchunguzi ufanywe wa lita za mafuta zenye gharama ya Sh. milioni 58, ushuru wake umelipwa wapi huku akiagiza bodi kutokana na unyeti wa kitengo cha usajili, ukaguzi na upelelezi wa walipakodi, kwamba kitendo hicho kijitegemee na kiripoti na kiwe chini ya Kamishna Mkuu na kisiripoti sehemu nyengine yeyote.

Alisema ukaguzi maalum unapaswa kufanyika kuchunguza utendaji wa mfumo wa ukusanyaji mapato ambao unaonekana unahujumiwa huku akitaka kufuatiliwa kwa akauti za benki ambazo mlipakodi hulipa ada ya bandari ili kujua hizo fedha za kampuni ya usafiri wa meli zimeingia katika akaunti gani.

Dk. Mwinyi aliongeza kuwa hatua hizo ndizo zinazosababisha utendaji wa kazi ufanyike kwa kiwango cha chini na kusema kwamba hatamwonea mtu ndiyo maana anataka kufanywe uchunguzi na ikithibitika waliotuhumiwa hawana kosa, haki itatendeka lakini ikithibitika wana makosa lazima sheria ifuate mkondo wake.

Rais Dk. Mwinyi alisema amepokea taarifa za kusikitisha kutoka kitengo cha uchunguzi cha bodi hiyo kwamba jukumu lake ni kufanya uchunguzi wa ulipaji wa kodi na kikishafanya uchunguzi, ni jukumu la ZRB kufanya uchunguzi zaidi wa taarifa hiyo lakini kinachotokea ni kuzimwa kwa uchunguzi huo.

Alisema baadhi ya mifano ni uchunguzi uliofanywa wa moja ya kampuni ya meli ya usafirishaji wa abiria ambao unaonyesha tofauti ya ulipaji wa Sh. bilioni 9.65 ambazo hazikulipwa wakati uchunguzi ulifanyika na ikaonekana kwamba mhusika amelipa lakini fedha hazikuonekana.

Mfano mwingine, alisema ni Mkurugenzi wa Usajili, Ukaguzi na Upelelezi wa Walipakodi, Hashim Kombo Haji, aliamuru ripoti hiyo iondolewe na isipelekwe katika uongozi lakini ilipelekwa kwenye uongozi na kilichofuata ripoti haikupelekwa kwenye bodi ambapo uongozi kwa kibali cha Kamishna Mkuu haukupeleka kwenye bodi hiyo.

Pia alisema kuna kampuni ya mafuta haikulipa kodi ya lita zenye gharama ya Sh. milioni 58 Tanzania Bara na uchunguzi ulifanywa na TRA na maelezo ya kampuni hiyo ni kwamba fedha hizo haziwezi kulipwa Tanzania Bara kwa sababu mafuta hayo yameletwa Zanzibar lakini baada ya Rais kuagiza kufuatiliwa kama kweli fedha hizo zimelipwa, ilionekana hazikulipwa sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Rais Dk. Mwinyi alisema ZRB ndiyo moyo wa serikali kwa kuwa ufanisi wake ndiyo unaoifanya serikali kutekeleza majukumu yake ya kimaendeleo na uendeshaji wake.

# Kampuni matatani kwa 'upigaji' TPA

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BUNGE limeitaka serikali ichukue hatua za kisheria kwa kampuni zote zilizosababishia hasara ya zaidi ya Sh. bilioni 3.2 na Dola za Marekani milioni 2.3 katika Mamlaka ya Bandari (TPA).

Vilevile, limeagiza watumishi wote wa TPA waliotajwa kushiriki mchakato wa ununuzi na usimikaji wa mfumo wa ERP wachukuliwe hatua kwa kuzingatia matokeo ya kiuchunguzi na uhusika wa kila mmoja katika mchakato huo.

Pia serikali itumie taasisi ya umma ya Wakala wa Serikali Mtandao (E – Government) kusimamia na kuratibu shughuli zinazoendelea za uwekaji mifumo ya TPA, ili kuongeza uwajibikaji na kupunguza gharama zilizoingiwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, alisema hayo jana bungeni alipowasilisha taarifa ya mwaka 2020/21.

Alisema kamati ilichambua taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kubaini kutokamilika kwa wakati mchakato wa usimikaji mifumo muhimu ya usimamizi na uendeshaji wa shughuli za TPA na kutokamilika kwa mfumo huo kumeishasababishia harasa serikali.

Alisema TPA ilikuwa imesimika mifumo zaidi ya 10 ambayo haikuwa inasomana, hivyo kutokuwa na tija na ufanisi kwa mamlaka.

Kaboyoka pia alisema TPA ilitoa tuzo ya mkataba wa kusimika mfumo wa ERP kwa awamu ya kwanza kwa Kampuni ya Soft Tech Consultant Ltd (STCL) kwa gharama ya Sh. 694,142,960 ambayo haikuwa na sifa na uwezo stahili, STCL ililipwa kiasi cha Sh. 600,433,963 sawa na asilimia 87 ya mkataba pamoja na mkataba husika kusitishwa, hivyo TPA ilipata hasara ya Sh. 600,433,963.

Alisema TPA iliingia mkataba wa nyongeza na STCL wa Dola za Marekani 31,860 kwa ajili ya mafunzo ya watumishi 165 licha ya mkataba wa awali kuhusisha mafunzo ya aina ileile.

Alisema kiasi cha Sh. 12,177,480 kililipwa zaidi isivyostahili kutokana na kubadilishwa sifa za vifaa vilivyopangwa kufungwa kwenye mradi, Kampuni ya Twenty Third Century Systems (TTCS) ilipewa tuzo ya mkataba Na. AE/016/2014-15/CTB/G/39 wa Dola 6,635,387.16 kwa upendeleo kwa kuwa haikuwa na sifa stahili.

Mwenyekiti huyo alisema mkataba huo pia ulivunjwa wakati TPA ikiwa imelipa kiasi cha Dola 4,632,099 sawa na asilimia 70 ya thamani ya mkataba wakati utekelezaji ukiwa kwa asilimia 42.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUONESHA NIA: KWA AJILI UTOAJI WA HUDUMA ZA UHAMISHAJI**
**KUMB NA. 10007512**

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini ya ardhi la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

Kama sehemu ya ufunguaji wa ofisi katika mkoa wa Dar Es Salaam, EACOP inatafuta watoa huduma za kusaidia shughuli za uhamishaji ofisi. Hivyo, EACOP inayaalika makampuni yenye uzoefu na yenye sifa stahiki kuonesha nia ya utoaji huduma za uhamishaji katika mkoa wa Dar es Salam.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
- Kusaidia kuweka mpango na ratiba ya uhamishaji ofisi.
- Kutoa usaidizi wa dharura wa kitaalamu wa uhamaji ndani ya jengo moja (kama vile toka ghorofa moja hadi jingine).
- Utoaji wa vifaa vya kusaidia katika uhamishaji (mfano vifaa vya kufungashia, maboksi, kamba nk.).
- Kufungasha, kuweka vitu kwenye maboksi na kutoa msaada wakati wa maandalizi.
- Kuhama kutoka jengo moja hadi jingine au ndani ya ofisi.
- Fidia ya bima ya uharibifu kutokana na uhamaji wa vitu au kutoka sehemu moja hadi nyingine
- Uorodheshaji na ufuatiliaji wa vitu vilivyohamishwa.

**VIWANGO VYA USALAMA NA MAHITAJI MENGINE:**
- Mtoa huduma akubaliane na kuthibitisha kwamba waajiriwa wake watatii kanuni za OSHA.
- Mtoa huduma ahakikishe wafanyakazi watatambulika ama kwa sare, vitambulisho, beji au vifaa vingine vya kujilinda kwa ajili ya usalama kwenye eneo la kazi (sehemu zote mbili yaani mahali pa kuhamishwa na pa kuhamishia) na azingatie mahitaji ya usalama wa jengo.
- EACOP haitaruhusu mfanyakazi yeyote ambaye hatakidhi matarajio haya kuingia katika eneo la kazi.
- Mtoa huduma atatakiwa kutoa Vifaa vya kujikinga vinavyohitajika kwa kila mfanyakazi wake (mfano viatu vya usalama, glavu na kofia ngumu pamoja na miwani ya usalama).
- Mtoa huduma atatakiwa kutoa nyenzo za usafilishaji kama vile, malori, matoroli, mikokoteni au vifaa vingine vya kiusalama vinavyohitajika ili kuhamisha vitu vizito.
- Mtoa huduma atachukua tahadhari kwa ajili ya kulinda vitu vinavyosafirishwa dhidi ya kuathiriwa na hali ya hewa (mfano jua, mvua…).

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi yakimbatanisha:
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha kuthibitisha kulipa kodi kwa mwaka uliopita
- Inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kanzidata ya EWURA ya Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kutuma maombi.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa makampuni ya ndani.
- Aoneshe rejea za uzeofu wa huduma alizowahi kufanya zinazofanana na huduma za uhamishaji wa ofisi au vitu.
- Kutoa taarifa ya fedha ya mwaka uliopita

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) kabla ya saa **11:00** jioni kwa saa za Afrika Mashariki (EAT), siku ya tarehe **Machi 3 2022.** Anwani ya Barua pepe sharti iwe na Kumb Na: **00110007512.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni) ya awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa kampuni za awali zenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Maombi yote ya kuonesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza

216710002

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA: UTOAJI WA HUDUMA YA WALINZI WA USALAMA NA HUDUMA ZA MAPOKEZI KATIKA OFISI YA DAR ES SALAAM**
**REJEA NO. 0010007504**

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, linayaalika mashirika yenye uzoefu na yenye sifa kuonesha nia yao ya kutoa huduma za ulinzi na mapokezi kwenye mradi wa EACOP Ofisi ya Dar es Salaam. Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa waTanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
- Kutoa huduma za ulinzi wa saa 24/7 kwa majengo ya ofisi.
- Kutoa huduma za mapokezi wakati wa saa za kazi – sharti awe anazungumza Kiingereza.
- Kutoa huduma za ufuatiliaji katika Chumba cha Udhibiti wa Usalama saa 24/7 - sharti awe anazungumza Kiingereza.
- Kutoa Msimamizi wa shughuli za Usalama aliye na bidii na mwaminifu.
- Kutoa huduma za taarifa za Kiusalama kwa Ukanda wa Afrika Mashariki, hasa Tanzania na Uganda.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi yakimbatanisha nyaraka zifuatazo:
- Uthibitisho wa ISO18788.
- Uthibitisho wa kuzingatia Kanuni za Kujitolea za Umoja wa Mataifa za Ulinzi na Haki za Binadamu (VPSHR).
- Uthibitisho kwamba taratibu za ajira zinaepuka kuajiri wafanyakazi wanaokiukaji haki za binadamu.
- Kuonesha uwezo wa kusimamia shughuli za usalama, kutoa mafunzo na kwamba anatekeleza sera thabiti ya Uwajibikaji kwa Jamii kwa mujibu wa kanuni za kazi za kitaifa.
- Sampuli ya vifaa vya mafunzo kwa walinzi, mtu wa mapokezi, mwendeshaji wa SCR, na msimamizi. *
- Sampuli ya uchunguzi wa Tukio, utaratibu wa kuripoti na fomu za vielelezo.
- Rejea ya huduma alizowahi kufanywa zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa uwezo wa kampuni kimtaji katika utoaji wa huduma.
- Uthibitisho wa leseni za Biashara na leseni zote za udhibiti au uidhinishaji unaohitajika ili kutoa huduma hizi.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha kuthibitisha kulipa kodi kwa mwaka uliopita.
- Wakati wa kuwasilisha maombi inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kanzidata ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) wakati wa kutuma maombi haya.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa makampuni ya ndani.

  Kumbuka; vifaa vya mafunzo vinapaswa kuwa sampuli tu, uwasilishaji wa mwongozo kamili wa mafunzo HAUTAKIWI. Hata hivyo, ni muhimu kujumuisha muhtasari wa mtaala (syllabus) na maelezo ya ratiba ya mafunzo/ratiba ya urejeaji mafunzo.

Kampuni zenye nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00** alasiri saa za Afrika Mashariki (EAT), **4th March 2022 .** Kichwa cha habari cha Barua pepe kiwe ni **0010007504.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni) ya awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa taasisi za awali zenye vigezo baada ya taasisi hizo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA). Maombi yote ya kuonesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza

216712101

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanawake endeleeni na ajenda ya 50 kwa 50

**MOJA** ya mikakati ambayo wanawake wamekuwa nayo kwa muda mrefu hususani baada ya kufanyika kwa mkutano wa nne wa kimataifa wa Beijing nchini China mwaka 1995 ni kutaka nafasi za uongozi au kwenye ngazi za maamuzi kuwa asilimia 50 kwa 50 kati ya wanawake na wanaume.

Ajenda hiyo ilipata msukumo mkubwa duniani kote kutokana na mkutano huo uliofanyika chini ya Mtanzania, Getrude Mongella, akiwa katibu kutokana na suala hilo kuwa moja ya maazimio yake.

Hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba, uongozi si misuli bali ni akili, hivyo na wao wana akili na wamekamilika kwa kila kitu kama wanaume na wana uwezo wa kuongoza, hivyo wasitengwe kwa kuangalia jinsi.

Ajenda hiyo ya wanawake tunaona ina ukweli ndani yake, sio siri kwamba uongozi ni akili, uzoefu uwezo wa kuongoza na si kutumia nguvu, na hilo sasa limeanza kudhihirika baada ya serikali nyingi duniani kuona mantiki na umuhimu wake, hivyo kuanzisha michakato ya kuwapa fursa nyingi za uongozi.

Kwa Tanzania suala hilo sasa linatekelezwa kwa kiwango kikubwa kwa mfano Rais Samia Suluhu Hassan anatokana na jinsi hiyo huku Spika wa sasa ni mwanamke pamoja na Baraza la Mawaziri kuwa na idadi kubwa ya wanawake zikiwamo wizara nyeti kama Ulinzi, Mambo ya Nje, Afya, Utumishi kwa kutaja baadhi. Wengine wakiongoza mikoa, wilaya pamoja na wakurugenzi wa wilaya. Tumeshuhudia jinsi ambavyo wameonyesha uwezo mkubwa wa kuongoza, hivyo tunadhani ni vyema wengine wakaiga mfano huo ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kupata uteuzi.

Rais Samia ameshasema kuwa atateua wanawake kulingana na vigezo bila kujali chama anachotoka, hivyo nasi tunaunga mkono maelekezo wanayopewa ya kuwataka kukuza vipaji vyao vya uongozi.

Wanaharakati wa kutetea usawa wa kijinsia, huwa wanasema kwamba kaulimbiu ya mwanamke akiwezeshwa anaweza, haipaswi kupewa nafasi kwa sasa, kwa madai kwamba wanaweza kujiwezesha wenyewe.

Tunadhani hiyo inatokana na kwamba wanajiamini, hivyo kwa kujiamini huko, tunashauri waendelee kuimarishana na kuhimizana kuchukua hatua mbalimbali za kunyanyuana ili kushika nafasi za uongozi.

Kwa njia hiyo, tunaamini kwamba wanaweza kutafutiana nafasi hata kwenye vyama vya siasa ili waongeze, kwani kama wanavyosema wao, uongozi si misuli bali ni akili na kweli wamedhihirisha hilo.

Rais amewateua kwa wingi, hivyo wito wetu ni kwamba wasimwangushe, bali iwe ni fursa ya kuonyesha kwamba wanaweza kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa maana ya tija na ufanisi kama wafanyavyo wanaume au hata kuwazidi.

Iwapo watatimiza majukumu yao kama inavyotakiwa, tunadhani kuwa watamfanya Rais azidi kuwaamini zaidi na kuendelea kuwateua kadri inavyowezekana na hatimaye ile asilimia 50 kwa 50 inaweza kufikiwa.

Kimsingi, uongozi wa nchi si wa jinsi moja bali wa wote ili mradi wahusika wawe na na sifa zinazotakiwa ikiwamo elimu, weledi, uadilifu, kujiamini , uzalendo na utu ambazo tunaona ni za msingi kwa ajili ya kutumikia umma wa Watanzania. Tumeshuhudia kuanzia awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi hii, wanawake wamekuwa wakiteuliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi, lakini awamu ya sita wamekuwa wengi zaidi.

Wingi huo unaonyesha ni jinsi gani ambavyo wameweza kuibeba ajenda hiyo vizuri, kuendelea kuaminiwa. Kutokana na hali hiyo, tunadhani ingekuwa vyema iwapo watahamasishana na kupigiana chapuo kwa wale wenye sifa na vigezo vya kuongoza ili wapewe nafasi.

Waswahili wanasema kwamba, 'umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu', hivyo tunaona ni vyema wangeendelea kushikamana na kuwezeshana wanapotafuta asilimia 50 kwa 50 na inawezakana wakafanikiwa kwani dalili zimeanza kuonyesha hilo.

Hata hivyo, pamoja na Rais Samia kudhihirisha kwa vitendo utashi katika kutekeleza ajenda hiyo kivitendo kwa kuteua wanawake katika ngazi mbalimbali, wanawake wasiridhike kwa nafasi za kuteuliwa pekee, bali waende pia kugombea udiwani kwenye kata na ubunge wa majimboni wachuane na wanaume ili idadi yao iongezeke katika vyombo vya kutoa uamuzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Machinga poleni kwa magumu, ndio safari ya mafanikio ilivyo

Na Anthony Gervas, Mwanza.

**KUNA** msemo 'mwanzo mgumu'. Ndicho kilichowakuta wafanyabishara ndogo maarufu machinga baada ya kuondolewa na serikali katikati ya miji na kupelekwa kwenye maeneo rasmi yaliyotengwa kwa ajili yao.

Mwaka jana serikali ilichukua hatua hiyo, ili kuondoa adha, misongamano na uchafuzi wa mazingira katika majiji na miji, hasa kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi kibiashara.

Niseme, kuna namna Serikali ina hoja kwa sababu wanawapigania haki yao kimaisha. Serikali inawajibika kuwahakikishia miundombinu mizuri inayohitajika, wateja waweze kufika katika maeneo hayo kuwajengea huduma za vyoo vya kudumu na vya kisasa.

Ukweli ni kwamba wengi walilalama sana kuhusu hatua hizo, kutokana na kudai maeneo waliyotengewa miundombinu yake na biashara bado siyo rafiki kwao kupata wateja.

Ni hoja zilizoenda mbali, kwamba hata fedha wanazofanyia biashara, ni mikopo kutoka kwenye taasisi za kibenki au fedha.

Ni kweli sehemu nyingi walizokuwa wametengewa zilikuwa bado hazijakaa vizuri kibiashara, hata kuwapata wateja ilikuwa 'shughuli pevu' kama vijana wa mjini wanavyotamka. Wateja bado ni adimu kulingana na mazingira yao, maana hawakuzoea kwenda walikopelekwa hao machinga.

Wapo machinga walioshindwa kuendelea na biashara mitaji yao ikikatika, wengine wakabadilisha mfumo wa kazi hiyo na huenda kuna wengine waliokimbia madeni ya watu au mikopo, kutokana na dai hilo la hali ngumu itokanayo na mabadiliko ya ghafla kibiashara.

Lakini hadi sasa, kuna kundi la waliokaza roho zao kwenda katika maeneo waliyopangiwa na serikali, wameshazoea maisha mapya ya kule, licha ya changamoto zinazowakabili kwenye shughuli zao.

Kama ilivyo hulka ya binadamu, nao wamebuni mbinu mbadala ya kupambana, ili mradi biashara iendelee. Wapo machinga ambao kuna sehemu wao wamebuni mbadala wa kurejea mjini nyakati za jioni kuendelea na biashara.

Hapo wanahesabiwa wauza viatu, nguo, bidhaa za majumbani na kwa hapa kwetu jijini Mwanza staili yao, wawapo kwenye biashara wanakuwa wamekaa chonjo. Jijini Mwanza kuna mtaa maarufu kama vile Makoroboi, uliokuwa umesheheni wafanyabiashara hao wadogo waliokuwa wakifanyabiashara nje ya maduka mengine, wakisababisha kuwapo mkanganyiko wa kukwepa kulipa kodi kwenye maduka makubwa.

Pia, baada ya serikali kugundua hilo, iliamua kufanya taratibu mzuri wa kuwabaini watu wa aina hiyo ili kila mmoja aweze kutekeleza wajibu wake wa kulipa kodi na serikali kupata mapato.

Ni muhimu serikali ikaendelea kuboresha miundombinu, ili kuwawezesha machinga hao wakuze mitaji yao na kuendeleza biashara ndogo na maisha ya kila siku wakiwamo wajasiriamali wengine wa aina hiyo.

Tunajua serikali ina nia njema ya kuwasaidia wafanyabiashara hao ambao wengine wanalalamika kwamba bado miundombinu haijawa rafiki kama inavyotakiwa, kutokana na maeneo mengine kuwa hayafikiki kwa urahisi kwa ajili ya wateja.

Tunaipongeza serikali kwa hatua ilizochukua kuweka mazingira mazuri ya majiji na miji, usafi, kupunguza misongamano na uchafuzi wa mazingira uliokuwapo kutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara.

Nami nawakumbusha wamachinga kuwa 'mvumilivu hula mbivu'. Wanatakiwa kuvumilia, lakini baadaye hali itaboreka na wateja wataweza kuzoea kwenda kununua bidhaa katika maeneo yao ambayo yamepangwa kwa utaratibu mzuri na serikali, hata watayaona matunda yake na faida ya kutengewa maeneo rasmi ya biashara.

Bado nakumbuka Rais aliwadokeza kwamba wawe wavumilivu, mambo mazuri yanakuja, Binafsi nasimama katika imani kwamba, hakuna kinachoshindikana chini ya maelekezo ya kiserikali, labda inapotokea bahati mbaya watendaji wasiowajibika vilivyo na daima husahihishwa.

Ni wajibu wa serikali ikachukua hatua zaidi kuhakikisha inawasaidia machinga, ambao kimsingi ni raia wake waondokane na kero za biashara ili kukuza mitaji, kama alivyoahidi mkuu wa nchi kuwajengea mifumo bora ya fursa za mikopo.

Awali wakati wakiondolewa katikati ya miji na majiji, paligeuka kuwa uwanja wa vita bayana ya machinga na serikali, mgambo wa jiji na polisi waliweza kupambana vikali

## Bosi Magereza akerwa matumizi hafifu ya rasilimali

**Na Idda Mushi,** MVOMERO

KAMISHNA Jenerali wa Magereza, Meja Jenerali Suleiman Mzee, ameeleza kutoridhishwa na baadhi ya magereza kushindwa kutumia rasilimali watu, vifaa na mazingira katika maeneo ili kubuni miradi ya maendeleo.

Jenerali Mzee alisema hayo baada ya kuzindua nyumba mbili kwa moja kwa ajili ya makazi ya askari katika Gereza la Vijana Wami, Mvomero mkoani Morogoro.

Alisema jeshi hilo liko tayari kusaidia taasisi zake yakiwamo magereza yatakayokuwa tayari kuanza kutekeleza miradi kwa nguvu zao kwa sababu rasilimali za kufanya hivyo zipo na hata maeneo kwa ajili ya uendelezaji pia yapo.

"Katika Magereza ambayo hayanifurahishi Tanzania ni haya mawili (Vijana Wami na Wami Kuu). Hamnifurahishi kabisa, haiwezekani mko wengi hivi halafu nyumba mliyojenga ni moja tu. Wenzenu wana nyumba 10 hadi 20. Isanga (gereza) wana nyumba 50, kikubwa ninachotaka ni mabadiliko. Nataka kuona maendeleo," alisema.

Mzee alilishauri Gereza la Vijana Wami kutumia rasilimali za majengo lilizo nazo kuanzisha chuo cha mafunzo ya ufundi, kwa vile wafungwa katika gereza hilo wamekuwa wakijifunza katika nyanja mbalimbali.

Alisema badala ya kutumika kuwafundisha wafungwa peke yao, watumie pia kufundisha raia wengine kwa sababu majengo na walimu wapo wa kutosha kwa ajili ya kazi hiyo.

"Wenzenu jirani na barabara wanaanzisha nyumba za kulala wageni, vituo vya mafuta, maeneo ya uwekezaji wa biashara, wanafyatua matofali. Kwani nyie mmezuiwa?" alihoji.

Baada ya kushiriki pia upandaji miti katika gereza hilo maalumu la vijana, alihimiza upandaji miti kuwa endelevu hususani miti ya matunda ili kusaidia afya za askari na wafungwa sambamba na kuwezesha kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Kiongozi huyo aliwapongeza wakuu wa baadhi ya magereza likiwamo la mahabusu Morogoro kukarabati magari ya zamani ambayo sasa yamekuwa na uwezo kusaidia utekelezaji wa miradi inayoendelea kubuniwa, ikiwamo ubebaji michanga na matofali kwenye miradi ya matofali na kazi zingine.

Mkuu wa Gereza la Vijana Wami, Kamishna Msaidizi Abdallah Misanga, alisema ujenzi wa nyumba hizo umetumia sehemu kubwa nguvu kazi na rasilimali kutoka kwa askari na wafungwa na serikali iliwapatia Sh. milioni 67 kuzimalizia.

Kuhusu ujenzi wa chuo cha mafunzo ya ufundi, alibainisha tayari wameanza mchakato wa kuomba usajili na wanaamini hadi mwakani watakamilisha na akatoa wito kwa wahisani mbalimbali kuwasaidia kupata vifaa katika karakana za kufundishia ili iwe rahisi kuendesha mafunzo.

# Serikali yalaumiwa kwa upotevu wa mabilioni

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BUNGE limesikitishwa na serikali kushindwa kutekeleza makubaliano yake ya kimkataba iliyoingia na Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC) kuhusu mauzo ya kiwanda cha viuadudu cha Tanzania Biotech Products limited (TBPL) Kibaha, mkoani Pwani kwa miaka mitano.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), Jerry Silaa, alisema hayo juzi bungeni wakati akiwasilisha taarifa kwa kipindi cha mwaka 2021.

Alisema hadi sasa serikali imekiuka matakwa ya kimkataba baina yake na NDC kupitia Wizara ya Afya uliotiwa saini Machi 11, 2015 ili kuwa na uhakika wa soko la ndani.

Kushindwa kutekeleza mkataba huo, alisema kumesababisha kupungua kwa mapato ya NDC, fedha ambazo zingeongeza uwezo wa shirika kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali pamoja na kuzalisha viuadudu kwa kiasi kikubwa.

Aidha, alisema kamati imebaini mkwamo mkubwa katika uwekezaji unaosababishwa serikali kushindwa kutekeleza matakwa ya kimkataba kati yake na NDC.

Alisema kiwanda hicho ni muhimu kwa mustakabali ya maisha ya watu na uchumi wa taifa lakini mkataba haukutekelezwa kutokana na serikali kutoweka kipaumbele na kutotenga bajeti kwenye halmashauri zake kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa hiyo.

Mwenyekiti huyo alisema kutokana na hali hiyo bunge linaitaka serikali kuhakikisha Wizara ya Fedha na Mipango inatenga fedha za kuiwezesha Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya 'technical Study' ya matumizi sahihi ya viuwadudu na kushughulikia kupatikana kwa ithibati ya Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kiwanda hicho.

Alisema itasaidia wizara kutumia fedha zinazotolewa na wahisani katika ununuzi wa viuwadudu vinavyozalishwa katika kiwanda hicho.

Pia alisema Wizara ya Fedha na Mipango itenge fedha mahususi katika kifungu maalumu (ring fenced) kitakachotumika kulipia ununuzi wa viuwadudu vya kuteketeza mazalia ya mbu vinavyozalishwa na kiwanda hicho, ili kukiwezesha kiwanda hicho kupata soko la ndani la uhakika, ikiwa ni pamoja na kuweza kurejesha mkopo uliotumika.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, Wizara ya Afya, itenge fedha kutoka vyanzo vyake kwa ajili ya ununuzi wa viuwadudu vinavyozalishwa na kiwanda hicho, ikiwa ni pamoja na kuhuisha mkataba baina yake na NDC.

Alisema ni muhimu kitengo cha biashara cha NDC kutafuta masoko kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), ili dawa zinazozalishwa katika kiwanda cha Tanzania Biotech zifahamike na uuzika katika nchi mbalimbali.

"Dhamira ya Kamati ni kuhakikisha kila senti iliyowekezwa na serikali inaleta tija iliyokusudiwa. Kwa mantiki hiyo, Kamati imekuwa ikifanyauchambuzi wa kina katika uwekezaji wa mitaji ya umma ili kubaini iwapo uwekezaji huo una tija na umefuata taratibu na miongozo mujarabu ya biashara,"alisema.




Mkurugenzi Mtendaji wa OreCorp, Matthew Yates (kulia), akikabidhi moja ya madarasa matatu mapya yaliyojengwa na kampuni hiyo kwa Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Veronica Kessy (kushoto), wakati wa hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika wilayani Sengerema, mkoani Mwanza. Mradi wa ujenzi wa madarasa hayo ni sehemu ya mpango wa kampuni hiyo wa kuiendeleza jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Shahidi akwamisha kesi mke wa Bilionea Msuya

**Na Kulwa Mzee**

KESI ya mauaji inayomkabili mke wa marehemu Bilionea Erasto Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyella, imekwama kuendelea kutokana na shahidi wa utetezi kwenye kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi kutofika mahakamani.

Shahidi huyo wa tatu alitakiwa kufika jana Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam mbele ya Jaji Edwin Kakolaki.

Inadaiwa shahidi huyo hakufika kwa sababu anaumwa, hivyo mahakama iliahirisha kesi hiyo hadi leo.

Katika kesi hiyo ndogo, mshtakiwa wa kwanza Miriam, kupitia Wakili wake, Omary Msemo, anapinga maelezo yake ya onyo kupokewa mahakamani kama kielelezo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuteswa wakati wa kuchukuliwa maelezo hayo ili akiri kuhusika na mauaji ya dada wa mumewe, Aneth Msuya.

Katika kesi hiyo tayari mashahidi watatu wa upande wa mashtaka wameshatoa ushahidi wao huku upande wa utetezi ukiwa umeshaleta mashahidi wawili ambao ni Miriam mwenyewe na mdogo wake, Mbazi Mrita.

Katika kesi ya msingi namba 103/2018, washtakiwa hao wanadaiwa kumuua kwa kukusudia Aneth Msuya, dada wa marehemu Bilionea Erasto Msuya Mei 25, 2016 maeneo ya Kibada wilayani Kigamboni, Dar es Salaam.

## Wizara: Asilimia 60 wanatumia tiba asili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya imebainisha kuwa zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania wanatumia tiba asili ili kujitibu dhidi ya magonjwa mbalimbali kabla ya kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Vilevile, imesema dawa 20 kati ya 73 zilizosajiliwa na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala zimeleta mafanikio makubwa kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Tiba wa Wizara ya Afya, Dk. Caroline Damiani, aliyasema hayo jana jijini hapa alipofungua mafunzo kwa waganga wa tiba asili yenye lengo la kubadilishana uzoefu na kujadili kero na mikakati mbalimbali ya kuikuza taaluma ya tiba asili na tiba mbadala ili iendelee kuwanufaisha Watanzania.

Alisema Watanzania hao wanapata tiba asili kwa ajili ya maradhi mbalimbali kabla ya kwenda katika vituo vya kutolea huduma au baada ya kwenda katika vituo ama hospitali zinazotoa huduma za kisasa.

Mkurugenzi huyo alisema hadi sasa Wizara ya Afya kupitia Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala imefanikiwa kusajili dawa za tiba asili 73, huku 20 zikiwa na mafanikio makubwa kwenye ugonjwa wa UVIKO-19.

Alibainisha kuwa dhima kuu ya mafunzo hayo ni kuhakikisha dawa zinazotengenezwa na Wataalamu zinakuwa bora kuanzia katika hatua ya uoteshaji, uvunaji, utengenezaji, uhifadhi mpaka hatua ya kumfikia mlaji ili isilete madhara kwenye afya ya mtumiaji

Alisema wamejadili njia bora ya kuhakikisha dawa za tiba asili zinapatikana kwa urahisi zaidi popote nchini na nje ya nchi ili kuwanufaisha wananchi na taifa kupata fedha za kigeni baada ya kuziuza nje ya nchi.

Aliwataka kuanzisha viwanda vya kutosha vitavyozalisha dawa za tiba asili, hali itayosaidia kuongeza upatikanaji wa dawa hizo katika maeneo mbalimbali nchini na kuwanufaisha wananchi.

Mkurugenzi huyo alitoa wito kwa waganga wa tiba asili kuzingatia maelekezo na maagizo ya wizara ili kushirikiana katika kutatua kero mbalimbali zinazoikumba taaluma hiyo.

Mwakilishi wa Waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala na Mbunge wa Lushoto, Shaban Shekilindi, alipongeza wizara kwa kuandaa mafunzo hayo kwa kuwa yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuwajenga na kukumbushana sheria na taratibu za taaluma ya tiba asili nchini.

Aliiomba serikali kuendelea kuinua taaluma ya tiba asili kwa kuwa waganga wengi vipato vyao ni vidogo kukidhi malengo yao ya kuwahudumia wananchi.

# Lukuvi akabidhi ofisi, ampa kongole Mabula

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

ALIYEKUWA Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amemkabidhi ofisi aliyekuwa naibu wake, Dk. Angeline Mabula, ambaye sasa ni waziri wa wizara hiyo.

Makabidhiano ya ofisi yalifanyika jana kwenye ofisi za wizara hiyo katika mji wa serikali Mtumba, jijini hapo.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Lukuvi alisema ana furaha kubwa kumkabidhi ofisi mtu anayeijua wizara na aliyekuwa akifanya naye kazi.

''Dk. Angela anayajua mengi kwenye wizara. Tumeshirikiana katika kushughulikia dhuluma na malalamiko ya ardhi na katika kipindi chote, tumejitahidi kupunguza malalamiko na yamepungua,'' alisema Lukuvi ambaye ni Mbunge Isimani.

''Ninaomba mumpe ushirikiano, nimefanya naye kazi takriban miaka sita na tumeelewana sana na nilimpa kazi nyingi kwa sababu ana uwezo. Tofauti yangu mimi na yeye ni kuwa mimi ni mkali yeye ni mpole,'' alisema.

Kwa mujibu wa Lukuvi, wakati wa uongozi wao, wizara ilipiga hatua kubwa katika masuala mbalimbali yakiwemo mabadiliko ya mfumo wa utunzaji kumbukumbu za ardhi sambamba na uanzishwaji ofisi za ardhi za mikoa.

Aliishukuru menejimenti ya wizara kwa kuonyesha ushirikiano wakati wa kipindi chote alichokuwa wizarani hapo na kuitaka menejimenti hiyo kumpa ushirikiano Waziri Mabula.

Dk. Mabula alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kumuamini na kumteua kuwa Waziri wa Ardhi. Pia alimshukuru Lukuvi kwa kumpa uhuru wa kufanya kazi wakati wote walipokuwa wakifanya kazi pamoja.

Alisema katika kipindi cha uongozi wao, wizara imefanya mambo mengi kwa lengo la kuondoa kero na changamoto za sekta ya ardhi na kubainisha kuwa mafanikio yote yalitokana na ushirikiano na menejimenti ya wizara.

''Mengi yamefanyika kuondoa changamoto kwa ushirikiano na timu nzima ya menejimenti. (Lukuvi) umenilea vizuri, malezi na imani uliyokuwa nayo ni wazi nina deni kubwa la kulipa katika utendaji kazi,'' alisema.

Waziri Mabula aliongeza kuwa pamoja na mambo mengine, msisitizo wa wizara yake kwa sasa ni vipaumbele vya Rais Samia katika masuala ya uwekezaji na mifumo ya utunzaji kumbukumbu za ardhi.

Lukuvi aliondolewa nafasi ya uwaziri katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri yaliyofanyika mapema Januari, mwaka huu. Alikuwa Waziri katika wizara hiyo tangu mwaka 2014 na amedumu kwa miaka nane.



Mkuu wa Wilaya ya Iramba mkoani Singida, Selemani Yusufu Mwenda, akizindua zoezi la upandaji miti katika kijiji cha Mayanzani, Kata ya Urughu, wilayani Iramba kwa kupanda mti kwenye eneo lililochaguliwa kwa ajili ya kupanda jumla ya miti 250,000. **PICHA: JUMBE ISMAILLY**

# Utata waibuka polisi kutaka kufukua kaburi dereva boda

**NA Frank Kaundula,** MOROGORO

HALI ya sintofahamu imeibuka katika familia ya Mzee Omary Siogope, mkazi wa kijiji cha Madoto, wilayani Kilosa baada ya kupokea taarifa kutoka Jeshi la Polisi wakitaka kufukua kaburi la mtoto wao, Habibu Omar (21).

Uamuzi wa polisi kutaka kufukua kaburi hilo umekuja ikiwa ni miezi miwili tangu Habibu azikwe baada kuuawa na watu wasiojulikana na kutokomea na pikipiki.

Akizungumza na Nipashe juzi, baba wa marehemu, Omary Siogope, alisema kijana wake alitoweka Novemba 14, mwaka jana kisha mwili wake kupatikana Desemba 11 ukiwa umetelekezwa katika mashamba ya mkonge akiwa ameshafariki dunia.

Siogope alisema baada ya kupatikana, mwili huo ulifanyika uchunguzi wa kidaktari chini ya jeshi la polisi lakini hawakupata majibu yoyote na hakukuwa na taarifa ya kiuchunguzi hadi walipopata taarifa ya kutaka kufukuliwa kaburi.

"Kabla ya mazishi polisi kwa kushirikiana na daktari, walichukua baadhi ya viungo vya mwili wa marehemu kwa madai ya kufanya uchunguzi lakini mpaka sasa hatujui hatua gani zimechukuliwa hadi wamerudi tena," alisema Siogope.

Hata hivyo, suala la kufukua kaburi lilishindikana kutokana na mvutano kati ya ndugu na polisi baada ya baba mkubwa wa marehemu, Ally Rajabu, kusema familia ilitaka jambo hilo kufanyika kwa uwazi tofauti na polisi waliotaka kufanyika kwa usiri.

Alisema sababu ya familia kutaka kuwapo kwa uwazi ni baada ya kutopatiwa taarifa za hatua zilizochukuliwa awali baada ya uchunguzi uliofanyika ili wawe na uhakika na kupatikata kwa haki ya mtoto wao.

"Hatujui hatua gani zimechukuliwa mpaka sasa kwa waliohusika na kifo cha motto wetu . Tunashangaa walituambia wanataka kufukua kaburi kwa ajili ya upelelezi. Sisi tunataka kuwe na uwazi ili tujue hatima ya wanaohusika wasifanye kwa siri," alisema Rajabu.

Akitolea ufafanuzi sakata hilo, Kaimu Kamanda Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi (ACP) Sospeter Kungura, alisema kilichokuwa kinatakiwa ni upelelezi wa kesi hiyo ambayo tayari watu wanne wanashikiliwa kwa tuhuma ya mauaji wa kijana huyo.

"Tunawashikilia watuhumiwa wanne kutokana na tukio hilo, kwa hiyo tuko kwenye upelelezi na hatuwezi kulizungumzia kiundani kwa sababu za kiuchunguzi," alisema Kungura.

# Uchimbaji madini endelevu kujadiliwa

**Na Romana Mallya**

WADAU sekta ya madini zikiwamo kampuni za uchimbaji, watengenezaji na wasambazaji wa mitambo watakutana kujadili uchimbaji madini endelevu na namna teknolojia zinavyoweza kuufanya uzingatie mabadiliko ya tabia nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi isiyo ya kiserikali ijulikanayo kama Policy Analysis and Development Organization (PADO), Prof. Sufiani Bukurura, alisema wadau hao watakutana chini ya Jukwaa la Uchimbaji Madini Tanzania (TAMFO).

Prof. Bukurura alisema kongamano hilo linatarajia kufanyika kwa siku mbili kuanzia Machi 9, mwaka huu jijini Mwanza na litajumuisha pia viongozi mbalimbali kutoka serikalini.

"Kongamano hili la kimataifa la uchimbaji madini litakutanisha kampuni kubwa, za kati na ndogo zinazojihusisha na uchimbaji madini, wachimbaji wadogo, kampuni za ndani na nje zinazotengeneza au kusambaza mitambo na teknolojia katika uchimbaji na wauzaji wa vito vya thamani," alisema.

Alisema mada ya mwaka huu ni "Uchimbaji wa Madini Endelevu ni namna gani teknolojia zinaweza kufanya uchimbaji wa madini uzingatie mabadiliko ya tabia nchi."

Prof. Bukurura alisema siku ya kwanza mbali ya hotuba za viongozi wa serikali na wadau kutakuwa na mawasilisho ya kitaalamu na midahalo.

"Mawasilisho yatajumuisha mada kama uwajibikaji katika uchimbaji wa madini kwa maana ya utunzaji wa mazingira; hali halisi kuhusu uchimbaji madini na mabadiliko ya tabia nchi na uchimbaji wa madini shirikishi na endelevu unaohusisha jinsia zote, vijana, wenye ulemavu," alisema.

Alisema siku ya pili ya kongamano itahusisha maonyesho ya teknolojia mpya zinazoweza kusaidia sekta ya madini iwe endelevu.

"Itaambatana na maonyesho ya namna uchimbaji unafanyika katika maeneo mbalimbali ya nchi. Tutaonyesha mahali tulipo na teknolojia ambazo pengine zingetumika na kuwezesha uchimbaji madini nchini ungekuwa rafiki zaidi," alisema.

Alisema tayari kampuni zaidi ya 10 za ndani na nje ya nchi zimethibitisha ushiriki kwenye TAMFO 2022.

Alisema Waziri wa Madini, Dotto Biteko na Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda, Ally Gugu, wanatarajia kushiriki katika jukwaa hilo.

"Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Tume ya Madini watashiriki. Tutakuwa na wadau wa sekta hii wakiwamo wahadhiri, wanaharakati na watafiti, tunaomba wadau wajumuike nasi ili kwa pamoja tutathmini sekta yetu iwe na uchimbaji endelevu," alisema.

BADO ni taasisi isiyo ya kiserikali inayojihusisha kufanya utafiti, mafunzo ya kivitendo na kufanyia tathmini sera na mipango ya serikali ili kutoa mchango katika kuhakikisha Tanzania inapata maendeleo endelevu.

## Asilimia 80 ya watoto wadogo hufanyiwa ukatili

**Na Yasmine Protace**

IMEELEZWA kuwa asilimia 80 ya watoto wadogo wanaongoza kwa kufanyiwa ukatili wa kijinsia.

Hayo yalisemwa na Asia Mkini, mkuu wa kitengo cha dawati la mkono kwa mkono kutoka Hospitali ya Mwananyamala jijini Dar es Salaam.

Asia ambaye alikuwa akitoa mada inayohusu, nyenzo za kukabiliana na ukatili, kwa washiriki wa semina za Jinsia na Maendeleo(GDSS), alisema matukio ya ukatili yanafanyika kwa watoto wadogo kwa kiwango kikubwa.

"Asilimia 80 ya matukio ya ukatili yanafanywa kwa watoto wadogo," alisema na kuongeza kuwa mtu yeyote anayefanyiwa ukatili anatakiwa kufika kituo cha mkono kwa mkono ili aweze kufanyiwa uchunguzi ikiwamo na kupatiwa matibabu ambayo hutolewa bure.

Alisema vituo vya mkono kwa mkono vinatoa huduma mpaka saa tisa mchana, lakini pamoja na ingawa katika hospitali huduma hiyo inaendelea kutolewa.

Christopher Neuton, kutoka Dawati la Jinsia na Watoto Kinondoni, alisema kuwa kuanzishwa kwa dawati ni kuwasaidia manusura kupata huduma bure pamoja na haki zao.

"Kuanzishwa kwa dawati kunawasaidia manusura kupata matibabu bure ikiwamo na kupata haki zao," alisema.

Aliongeza kuwa mtu yeyote ambaye anayafanyiwa ukatili wowote hatakiwi kuharibu ushahidi, kwani kuharibu ushahidi kuna sababisha mtuhumiwa kushinda kesi.

Alisema kuanzishwa kwa dawati kunasaidia kukamata wahalifu wote kwa mujibu wa sheria.

Pia aliwataka wazazi na jamii kutoa ushirikiano kwa polisi au watu wa madawati ya kijinsia ili wahusika wachukuliwe hatua.

Hassan Hamis, mshiriki wa GDSS, alisema wanaiomba serikali iweke vituo vya mkono kwa mkono ambavyo vinatembea ili kuwasaidia manusura kupata huduma kwa haraka.



Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro, akijaribu moja ya pikipiki 10 zenye thamani ya shilingi milioni 51.3, zilizotolewa juzi na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), kwa ajili ya kusaidia operesheni ya kupinga ukatili wa kijinsia nchini. Kulia ni mwakilishi wa shirika hilo, Georgette Kyomba, aliyekabidhi pikipiki hizo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Udongo mikoa wazalishaji wakuu taabani

**Na Gerald Kitabu**

UTAFITI wa afya ya udongo uliofanywa katika mikoa ya nyanda za juu kusini umebaini kuwa, udongo wa maeneo hayo, umechoka na hauna virutubisho muhimu kwa mimea, hali inayopunguza tija.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo -TARI Uyole kwa kushirikiana na kampuni ya OCP ya Morocco imetafiti na kubaini kuwa udongo wa mikoa ya Mbeya, Iringa, Songwe, Rukwa na Morogoro kwenye uzalishaji chakula, umepoteza zaidi ya asilimia 50 ya virutubisho miaka ya karibuni.

Hali hiyo inasababiha wakulima kukosa tija katika mazao ya mahindi, alizeti, viazi pamoja na mpunga katika maeneo mengi.

Akitoa matokeo, kiongozi wa utafiti huo Fredrick Mlowe, kutoka TARI Uyole alisema utafiti huo umeonyesha kuwa kuna upungufu mkubwa wa virutubisho vya 'naitrojeni, fosforas, solfur boron na zink.'

Alisema utafiti ulifanyika katika mashamba ya wakulima wadogo wa vijiji 100 vya kila kwenye mikoa ya Mbeya, Iringa, Songwe, Rukwa na Morogoro.

"Katika mikoa yote tumebaini kuwa udongo umechoka hautoi virutubisho vyote vya msingi kwa mazao, ambavyo mmea unahitaji ambavyo ni 13, lakini maeneo mengi viwango hivyo vipo chini kabisa," alisema Mlowe.

Alivitaja kuwa 'zink, salfa, naitrojen, boron,' na kuongeza kuwa katika virutubisho hivi zink imepungua zaidi mkoa wote wa Morogoro.

"Upungufu umeathiri wakulima wadogo kwenye mazao makuu ya mahindi, mpunga, viazi na alizeti."

Mlowe aliwashauri wakulima kutumia mbolea yenye virutubisho vyote muhimu na kampuni za mbolea kuzalisha mbolea yenye virutubisho vyote muhimu wakulima waongeze uzalishaji na tija

Utafiti huo ulionza mwaka 2019 na kumalizikia katika mkoa wa Morogoro hivi karibuni, ulisisitiza wakulima kuboresha afya na matumizi ya udongo kwa kuweka mbolea yenye virutubisho vyote muhimu.

"Katika utafiti huu tulishirikiana na kampuni ya OCP ya Morocco, viongozi wa mikoa na serikali za mitaa kufikia wakulima 10,000 katika vijiji 100," alisema Mlowe.

"Madhumuni ya utafiti huu ni kutoa majibu ya namna gani wakulima wanaweza kuongeza uzalishaji wa tija kwenye mahindi, mpunga, alizeti kwa kutumia mbolea," aliongeza.

Akitoa mapendekezo ya matumizi ya mbolea, Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alishauri wakulima watumie mbolea yenye virutubisho muhimu ikiwamo zink, salfa, naitrojen na boron na kutaka kampuni za mbolea kujikita kwenye eneo hilo.

Meneja wa kampuni ya OCP Tanzania, Dk. Mshindo Msolla, alisema kwa miaka mingi wakulima wamekuwa wakihangaika kufikia uzalishaji wenye tija.

Alisema serikali kwa kushirikiana na kampuni hiyo walianza kupima udongo mwaka 2019 na upiaji huo ulizinduliwa na Waziri wa Kilimo wakati huo Japhet Hasunga kule Vwawa mkoa wa Songwe na kuendelea Iringa, Mbeya, Rukwa na Morogoro.

Aliwashauri wakulima kuzingatia kanuni bora za kilimo, mbolea yenye virutubisho na kufuata ushauri wa wataalamu ili kuongeza uzalishaji na tija

Juma Mdeke kutoka Wizara ya Kilimo alisema ni faraja kwa serikali baada ya kutambua afya ya udogo mikoa minne na kwamba utafiti utawaongezea wakulima uelewa wa afya ya udongo ili kuongeza uzalishaji.

# Serikali yafanya tathmini mikopo makundi maalum

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeanza kufanya tathmini ya utoaji wa mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Uamuzi huo ulitangazwa jana bungeni wakati ofisi hiyo ilipojibu swali la Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei.

Katika swali lake, Dk. Kimei alihoji kama serikali inaweza kutoa tathmini ya urejeshwaji wa mikopo inayotolewa na halmashauri kwa vikundi vya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu katika kipindi cha angalau miaka mitatu iliyopita.

Kwa mujibu wa ofisi hiyo, tathmini hiyo ilianzia tangu kuanza kutumika kwa sheria mwaka 2018/19 hadi Desemba 2021 kwa kuzielekeza halmashauri zote kuwasilisha taarifa ya mikopo na marejesho iliyotolewa tangu kuanza kwa sheria kupitia barua yenye Kumb.Na CB.352/428/01/8 ya tarehe 04/01/2022.

Ilisema taarifa za awali baada ya uchambuzi zinaonyesha kuongezeka kwa vikundi katika kurejesha mikopo hiyo.

Hata hivyo, ilisema taarifa hizo bado zinahakikiwa zaidi kwa kukaa na halmashauri na mikoa ili kupata viambatisho muhimu ili kuwa na uhakika wa usahihi wa taarifa hizo ambazo zitatolewa rasmi. Ilisisitiza imeshaanza kuboresha mfumo kwa kuandaa mwongozo wa usimamizi wa mikopo hiyo ambao upo katika hatua za mwisho za uidhinishwaji.

Vilevile, Ofisi ya Rais -TAMISEMI pia imeshasanifu mfumo wa kielektroniki utakaowezesha usimamizi madhubuti wa mikopo katika usajili wa vikundi, utengaji wa fedha, utoaji wa mikopo, usimamizi wa marejesho na shughuli za vikundi katika mamlaka za serikali za mitaa.



Mbunge wa Viti Maalum, Jacqueline Kainja, akiuliza swali bungeni jijini Dodoma jana, ambapo aliuliza je ni lini serikali itajenga hospitali ya kanda ya magharibi kama ilivyoainishwa katika ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). **PICHA: IBRAHIM JOSPEH**

# Wizara yaja na mkakati wa kusaidia wachimbaji

BUNGE limeelezwa kuwa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) limeandaa mkakati maalumu kwa ajili ya kuwasaidia na kuwaendeleza wachimbaji wadogo nchini ikiwamo wa Mkoa wa Njombe.

Wizara ya Madini ilibainisha hayo bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Njombe Mjini (CCM), Deodatus Mwanyika.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itaanza kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini katika Jimbo la Njombe Mjini kama inavyofanya kwenye maeneo mengine.

Wizara hiyo ilisema katika kuwasaidia wachimbaji wadogo, kupitia shirika hilo imeandaa mkakati maalumu ambao umeanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2021/22 na umejikita kwenye maeneo manne muhimu.

Ilitaja maeneo hayo ni mpango wa mafunzo kwa mwaka mzima ambao utafanyika nchi nzima na uliandaliwa kwa kushirikisha wachimbaji wadogo kupitia uwakilishi wa vyama vyao (FEMATA) na ambao kwa sasa upo tayari kwa utekelezaji.

Ilisema mafunzo hayo yatatolewa kwa kuhusisha taasisi mbalimbali zinazohusika na utozaji wa tozo na kodi kama Mamlaka ya Mapato (TRA), Tume ya Madini na halmashauri.

Pia ilisema mpango wa kuwawezesha wachimbaji wadogo kukopesheka katika taasisi za fedha ambapo tayari shirika limeishaingia makubaliano na taasisi za fedha za CRDB, NMB na KCB ambazo zipo tayari kuwakopesha wachimbaji hao.

Ilibainisha eneo lingine ni kuingia makubaliano na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) ambayo itawasaidia wachimbaji wadogo kujua taarifa za mashapo katika maeneo yao kabla hawajaanza kuchimba na kupata mitambo ya uchorongaji mahususi kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kwa kuanzia shirika limeagiza mitambo mitano ya uchorongaji.




Habari zote na Augusta Njoji

## Bilioni 2/- kununua magari kuzima moto

JESHI la Zimamoto na Uokoaji limetengewa bajeti ya Sh. bilioni mbili kwa mwaka 2021/22 kwa ajili ya kununua magari mapya ya kisasa ya kuzima moto.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilibainisha hayo bungeni jana ilipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko, aliyetaka kujua lini serikali itanunua magari ya kisasa ya Zimamoto ili kunusuru maisha ya raia na mali zao.

Ilisema lengo kuu la ununuzi wa magari hayo ni kuongeza ufanisi kwenye shughuli za kuokoa maisha na mali za wananchi pindi patokeapo ajali za moto na nyingine.

Wizara hiyo ilisema taratibu zote za ununuzi zikikamilika, magari ya kuzima moto yatapelekwa katika mikoa isiyokuwa na huduma ya zimamoto na uokoaji.

Hata hivyo, ilisema serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka ili kuliwezesha vitendea kazi stahiki Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Ilisema serikali imeandaa mpango mkakati wa kuimarisha huduma ya zimamoto na uokoaji nchini kwa kuimarisha na kuongeza vifaa vya kisasa vya utendaji kazi katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Ilisema vifaa hivyo vya kisasa vitaenda sambamba na upelekaji wa huduma ya zimamoto na uokoaji katika wilaya zote ambazo hazina huduma hiyo.

## Mashamba madume bora ya ng'ombe kuimarishwa

MBUNGE wa Bahi (CCM), Kenneth Nollo, amehoji mpango wa serikali wa kujenga kituo cha uzalishaji wa madume bora ya ng'ombe wilayani Bahi ili kuleta tija kwa wafugaji na kukidhi mahitaji ya soko.

Ikijibu swali hilo bungeni jana, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilisema mpango wa serikali ni kuimarisha mashamba yake ya uzalishaji wa madume bora ya Mabuki - Mwanza, Kitulo – Njombe na Sao Hill lililoko mkoani Iringa ili kuzalisha madume mengi na bora kwa lengo la kuyasambaza kwa wafugaji wote wanaohitaji ikiwa ni pamoja na wafugaji wa Wilaya ya Bahi.

Pia ilisema serikali inaendelea kusisitiza matumizi ya teknolojia ya uhimilishaji katika kuboresha kosafu za ng'ombe ili kuwa na kundi la mifugo yenye tija katika uzalishaji wa nyama au maziwa na hivyo kukidhi mahitaji ya soko.



Ukurasa 12

TANROADS Singida inavyomudu kufungua mkoa kwa mitandao barabara kusikopitika




Ukurasa 13

Watanzania mmeamua kuvaa koti la Uviko-19?

BUFE

IJUMAA FEBRUARI 18, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

**CRB yakusanya makandarasi wazawa kuwajengea uwezo wawafikie wageni**

JOHN NAHIMANA:

# Elimu kidato cha pili Afrika, Mhadhiri wa Kunyoa Chuo Kikuu cha Marekani

## • Tuzo kibao, maarufu akifunza majimboni

**JOHN NAHIMANA**

MTU anaweza kuja na hoja kuwa kazi ya kinyozi ina uhusiano wa namna fulani kwa anayetumikia kutokuwa na elimu kubwa sana kama ilivyo dhana inayotawala.

Inawezekana kukawepo ukweli, lakini unapoangaliwa kwa kina katika maisha ya kinyozi bingwa ughaibuni, John Nahimana kuna ama 'ukweli' na ' sio ukweli' kwa lugha nyepesi na tamathali yake ni '50 kwa 50'.

Hiyo ni kwa sababu Nahimana, elimu yake hana hata cheti cha kuhitimu sekondari, lakini amepewa darasa la kufundisha taaluma hiyo ndani ya chuo kikuu.

Nahimana anafundisha unyoaji nywele katika chuo kikuu nchini Marekani, akielekeza kwamba alianza kazi yake, ambayo msingi wa ujuzi unaanzia kujaribu kimasihara. Wakati huo alikuwa makazi katika Kambi ya Wakimbizi Kanemba, akitumia mkasi na baadaye akawa mjuzi hata kumuingizia kipato.

"Eti nilianza kunyoa kiutani halafu baadaye ilinisaidia kununua mafuta ya taa ili niweze kusoma, nikaweza kununua hata baiskeli kwenda shule," anasimulia Nahimana na kuendelea "wakati huo nilikuwa natumia mkasi mmoja."

Anaeleza nyendo za maisha yake baada ya muda fulani akahamia katika kambi za wakimbizi katika nchi nyingine nyingi, kama vile nchini Malawi, Msumbiji, Zimbabwe na Afrika Kusini, kote akidumisha taaluma yake ya kunyoa watu nywele.



John Nahimana; raia wa Burundi aliyegeuka kinyozi na mtaaluma wa fani hiyo, maarufu nchini Marekani. **PICHA: MTANDAO**

Pia, anasema mara nyingi katika sehemu alizozunguka, alifanya kazi hiyo na watu wengine, isipokuwa katika nchi za Afrika Kusini na Malawi ndio akawa na saluni zake.

Nahimana anasema wakati wote huo, alikuwa akifanya kazi ya kunyoa huku anasoma shule na hata alipohitimu anaeleza mafanikio yake kuwa "Niliporudi Malawi kutoka Afrika Kusini, ndipo niliponunua gari langu la kwanza kutoka kwenye kipato cha kunyoa."

Nahimana anasema kwamba kadri siku zilivyoenda, alizidi kuyaona mafanikio kwani baadaye akapiga hatua zaidi ya maendeleo, akinunua gari la pili huku akiendelea kunyoa watu.

**MAPYA MAREKANI**

Anasimulia, baadaye alipata nafasi ya kwenda nchini Marekani ambako hapakuwa rahisi kuendelea na kazi hiyo ya kunyoa, kwani sharti la kumiliki saluni binafsi, alihitajika kuwa na cheti cha taaluma hiyo.

Kinyozi Nahimana anasema kwa kuwa alitoka Afrika akiwa na elimu ya kidato cha pili, akalazimika kuingia tena darasani kwa kozi ya kunyoa kwenye chuo kikuu kwa muda wa mwaka mmoja.

Anasema, masomoni na baada ya masomo akaonyesha umahiri mkubwa kitaaluma, hata akapatiwa jukumu la ukufunzi mahsusi akianzia jimbo la Idaho nchini Marekani, akiwanoa kwa kozi hiyo katika shule ndani ya eneo hilo tajwa.

"Kwa sasa naenda kusaidia kufundisha katika majimbo mbalimbali kama Arizona na Colorado," anasimulia, huku akidokeza ameshatunukiwa tuzo mbalimbali kutokana na umahiri wake katika taaluma hiyo.

Nahimana anazitaja baadhi ya tuzo kuwa ni 'kinyozi bora' katika jimbo analoishi na nyingine ni katika Chuo Kikuu cha Phoenix jimboni Arizona, mwaka huu.

UCHUMI

# TANROADS Singida inavyomudu kufungua mkoa kwa mitandao barabara kusikopitika

**Na Elisante John,** Singida

• Meneja wake aainisha mpangilio hesabu ya ushindi • RC Dk. Mahenge adokeza ishara ya neema inayokuja • Neema inayoendana na zama mpya za madini mkoani



Barabara iliyojengwa kwa kiwango cha lami iliyoko Singida, ikiwa ni sehemu ya zinazoiunganisha na mikoa jirani. **PICHA ZOTE: ELISANTE JOHN**

KWA anayeujua mkoa wa Singida, hapana shaka ana neno la kukiri kwamba hivi karibuni, kwamba miundombinu yake ya barabara imeboreka kwa kiasi kikubwa, kutokana na kasi iliyopo ya ujenzi wa miradi mikubwa, hususan barabara kubwa zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

Ni maboresho yanayoufungua mkoa huo wa katikati ya nchi, katika ramani kuu ya mawasiliano kitaifa na kimataifa.

Hapo inaibuka nadharia nyingine kuhusu mkoa kukwea kiuchumi katika ngazi zote; mtu mmoja mmoja, familia, hata taasisi na mashirika makubwa na sekta, kote kukishuhudiwa tija.

Ni nafasi inayofungua mlango unaohusu Ofisi ya Meneja wa TANROADS inayohudumia kilomita 1,716.12 za barabara kuu za mkoani kilomita 488.73 za lami, ambazo ni sawa na asilimia 28.5, ya kilomita zote za Singida.

Katika nadharia hiyo ya biashara na uchumi, kuwapo barabara zenye kiwango cha lami ndani ya mkoa, inaweka hatua muhimu ya kushawishi uwekezaji ambao jamii yake imejikita zaidi kwenye shughuli za kilimo na ufugaji.

Pia, hivi sasa mkoa umefungua na kupanua njia zaidi za shughuli za uchimbaji madini, ikiwamo dhahabu inayopatikana Ikungi na almasi Iramba.

### MIRADI ILIYOKO JIKONI

Erick Christopher ni Kaimu Meneja wa TANROADS Mkoani Singida, kupitia kikao cha Bodi ya Barabara, anaeleza hatua ya Rais Samia Suluhu Hassan kuupatia mkoa fedha nyingi ambazo zimechangia kuboresha mioundombinu ya barabara za mkoa.

Anatoa mifano kadhaa inayojumuisha ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti lililokamilika kwa gharama ya zaidi ya Sh. Bilioni 25 ni umeufanya mkoa kufunguka na mawasiliano yake kurahisishwa.

Pia, anadokeza hatua za neema zinafuata kwa barabara za Kaskazini mwa mkoa kupitia katika wilaya ya Mkalama, zitajengwa kwa kiwango cha lami, ili kuiunganisha Singida na mkoa jirani wa Simiyu, pia iliyoko katika Kanda ya Ziwa.

Erick, ambaye kitaaluma ni mhandisi, anasema barabara inayounganisha mkoa wa Singida hadi kufika Mbeya, ujenzi wake utaanza hivi karibuni, huku inayopita Manyoni - Itigi hadi Tabora, tayari umeshakamilika, hata kurahisisha uchukuzi wa mizigo na abiria

> **Katika mwaka wa fedha uliopo na ujao 2022/2023, eneo la maingiliano ya daraja la Mto Sibiti kilomita 25, yatajengwa, ikihusishwa kwenye mradi mkubwa kitaifa.**



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa daraja la msingi katika wilaya ya Mkalama, ambalo linatarajiwa kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 10.

Anataja miradi ya kitaifa ambayo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika, akitaja ni inayokatiza Karatu-Mbulu- Haydom- Sibiti- Lalago hadi Masw, yenye jumla za kilomita 389-Serengeti.

Kaimu Meneja Erick anataja barabara nyingine ya urefu wa kilomita 328 inayounganisha Kolandoto - Lalago-Mwanhuzi hadi Olden B, anasema ujenzi wake umeshaanza kwenye baadhi ya maeneo.

Anasema, barabara hizo zote kwa sehemu kubwa zimekatiza kwenye eneo kubwa la wilaya ya Mkalama, ina matarajio miundombinu yake ikikamilika itachochea maendeleo ya kiuchumi kwa jamii ya Singida na hata mikoa jirani.

Kaimu Meneja mhandisi Erick anasema barabara ya Rungwa-Itigi hadi Mkiwa (Ikungi Km 219), itakayounganisha Singida na mkoa wa Mbeya, tayari usanifu umekamilika na Daraja la Sanza lililopo katika wilaya ya Manyoni, nalo pia usanifu wake umekamilika.

Mtaalamu huyo wa ujenzi anataja barabara nyinginezo za urefu wa kilomita 93, usanifu



Kaimu Meneja wa TANROADS mkoa wa Singida, Mhandisi Erick Christopher.

wake unaendelea. Inakatiza katika maeneo ya Njuki - Ilongero - Nkungi hadi Haydom mkoani Manyara Pia, kuna kilomita 460 inayofika katika barabara ya Handeni (Tanga) -Kwamtoro - Kibrashihadi, yenyewe usanifu wake umekamilika na imeanza kujengwa kutokea mkoani wa Tanga.

Aidha, anasema kuna mradi mdogo wa maendeleo wa ndani unaoendelea kutekelezwa wa daraja la msingi lililopo katika wilaya ya Mkalama, lenye thamani ya zaidi ya Sh. Bilioni 10.933, utekelezaji umefikia asilimia 53.8.

Kaimu Meneja anataja miradi mingine midogo inayotekelezwa kazi ya usanifu imekamilika ni za Sabasaba (Singida Mjini) na Sepuka hadi Kizaga (Wilaya Iramba) zote zikiwa na jumla ya urefu kilomita 77.6.

Anataja zile ambazo usanifu unaendelea zikiwa na urefi jumla ya kilomita 89, ni kati ya Mkalama- Gumanga - Nduguti hadi Iguguno Shamba.

Pia, Kaimu Meneja huyo wa TANROADS anautaja mradi wa barabara ya Ulemo - Kinampanda hadi Gumanga na barabara ya 'Singida Bypass' yenye kilomita 46, ikipita pembezoni mwa mji, kazi ya usanifu wake inaendelea.

Anasema katika mwaka wa fedha uliopo na ujao 2022/2023, eneo la maingiliano ya daraja la Mto Sibiti kilomita 25, yatajengwa, ikihusishwa kwenye mradi mkubwa kitaifa.

Anarejea mradi mwingine wa kitaifa unaosimamiwa na wakala huo, ni ujenzi wa barabara ya Rungwa (mpakani mwa Mbeya na Singida) - Noranga -Itigi hadi Mkiwa, ambao zabuni yake imetangazwa kumpata mkandarasi.

### WABUNGE WATABASAMU

Mbunge wa Manyoni Magharibi (Itigi), Yahaya Masare, anasema barabara hiyo ina mafanikio hivi sasa, nyingi zinapitika huku akiomba kasi iongezwe katika miradi mikubwa ya barabara.

Anaitaja Rungwa (mpakani mwa Mbeya na Singida) - Noranga- Itigi hadi Mkiwa (Ikungi), akiomba ijengwe kiwango cha lami, ili kufungua mawasiliano ya uhakika baina ya mikoa ya Singida na Mbeya.

Masare anasema barabara hiyo pia inaleta manufaa ya kiuchumi kwa mkoa jirani Tabora, unaopakana na wilaya ya Manyoni. Anasema wilaya ya Mkalama iliyoanzishwa mwaka 2013, ikimegwa kutoka Iramba, imekosa mawasiliano ya uhakika na hali huwa mbaya kipindi cha masika.

Mbunge wa Singida Mjini, Mussa Sima, anapongeza juhudi za Tanroads Singida, kupitia fedha za serikali, katika kurahisisha miundombinu ya barabaraza mkoa wa Singida, hivyo kupitika muda wote wa majira ya mwaka, ikiwamo nyakati za masika.

Anaiomba Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), kuiga ufanisi anaoushuhudia kwenye barabara zinazohudumiwa TANROADS.

### KIBWAGIZO CHA RC

Mkuu wa Mkoa Dk. Binilith Mahenge, anasema, ujenzi wa barabara hizo kuu zitakapokamilika, zitafungua fursa za kiuchumi kwa jamii kitaifa, hivyo anaiomba jamii kuhakikisha inaendelea kushirikiana na serikali katika kutunza na kuilinda miundombinu inayojengwa.

Hapo anaitaja, baadhi ya moundombinu hiyo kuwa ni ya barabara, elimu, afya na maji, lengo ni kuleta tija zaidi baadaye kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Kwa mujibu wa Dk. Mahenge, hivi sasa mkoa wa Singida umefunguka kwa sehemu kubwa, kutokana na kuwapo mawasiliano ya uhakika ya barabara na hata zinazotarajiwa, zitaendelea kuufanya mkoa wa Singida kitovu cha maendeleo.

Kwa mujibu wa Kaimu Meneja Mhandisi Erick, TANROADS Singida, inahudumia jumla ya kilomita 1,716.12 za barabara kuu na barabara za mkoa, kati yake kuna kilomita 1,227.39 za changarawe na kiwango cha lami ni kilomita 488.73.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Watanzania mmeamua kuvaa koti la Uviko-19?






NA JOSEPH KULANGWA
+255 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

MAISHA utotoni kweli yana michezo mingi ya kitotototo. Ipo ya kukimbiakimbia na kukimbizana, ipo ya kujificha, mingine ya kujipikilisha na hata ya kibababababa na kimamamama.

Yote hiyo hufanyika kupitisha muda tu wa kujipanga kula na kulala. Ni dhima ya mtoto kula na kulala, akitegemea wazazi wake kwa asilimia 100 na si sheria ya kutunga bungeni, bali ya asili na kimaumbile.

Katika michezo hiyo, siku moja nakumbuka tukicheza nyumbani karibu na mlingoti wa chuma uliozingirwa na majani makavu, ambamo pia kulikuwa makazi ya sisimizi wakubwa ambao wengine wakiwaita sungusungu au chungu.

Ni wadudu wang'atao kwa uchungu mkali sana. Hivyo, siku hiyo baada ya mmoja wetu kung'atwa nao, tukaamua kwa pamoja bila kikao rasmi kuyachomelea mbali yale majani kwa matumaini ya kuwaua wale wadudu.

Mmoja wetu alikimbilia nyumbani kwao na kurudi na kijinga cha moto, ili kukamilisha kazi hiyo. Tulipowasha moto, wale wadudu haraka haraka wakaparamia mlingotini, kwa mwendokasi wa ajabu na punde tu walishafika kileleni mwa mlingoti ule.

Mara tukaona tusichoamini, wanashuka kwa kasi ileile kurudi chini, lakini wakiishia katikati ya mlingoti. Kumbe kule kileleni kulikuwa na joto la ajabu, kwani muda ulikuwa ni mchana wa jua kali.

Hivyo kileleni joto lilikuwa la kuua mtu na mdudu. Kwa kuwa chini nako kulikuwa na moto wakabaki katikati wakizingira mlingoti ule. Hakuna kushuka wala kupanda. Wakabaki hapo, nasi tukiwacheka kuwa wamekwama.

Ilifika jioni mpaka kiza kuingia, hawakuwa wameshuka wala kupanda. Nasi tukawa tumeitwa nyumbani kutekeleza jukumu la kula na kulala. Tukawa tumesahau ya siku hiyo, kwani ilishapita. Kulipokucha, kesho yake tuliporudi kwenye mlingoti hatukukuta mdudu hata mmoja.

Bila shaka walisubiri kukapoa, wakashuka na kutafuta hifadhi sehemu nyingine salama kwao. Naaamini waliondoka na funzo, kuwa si kila mahali ni pa kukimbilia bila kujua kuna nini uendako. Chini moto na juu moto, ila kati baridi isiyoaminika.

Simulizi hii inaakisi kinachotokea Tanzania leo. Mwanzo katika mwaka wa 2019 mpaka mwaka juzi, nchi kama sehemu ya Dunia, iliingia katika msukosuko wa Uviko-19, yaani zile nyika chini ya mlingoti zilishika moto.

Katika kupambana na ugonjwa huo, wataalamu na viongozi wakasema tupande juu ya mlingoti; tuvae barakoa, tunawe maji tiririka na sabuni, tutumie vitakasa mikono na tujiepushe na misongamano au mikusanyiko. Tulifuata tukasubiri katikati ya mlingoti palipo na baridi.

Tumekaa hapo mpaka kuona kwamba yawezekana juu hakuna joto tukwee zaidi, tumetupa barakoa, hatunawi maji tiririka na sabuni, hatujitengi na mikusanyiko, tunapuyanga kana kwamba hakuna Uviko-19 tena, sasa tunaonekana kujongelea kilele cha mlingoti, bila kujua nako kuna joto.

Maana yake bado inasimama kwamba Uviko-19 upo, haujaisha na unaua. Tunajiaminisha katika mtazamo eti utaishi kwa adabu!

Nenda katika mikusanyiko, iwe mikutano, semina, makongamano na kadhalika, kinachoonekana sasa ni kwamba ukivaa barakoa unaonekana kama mtu aliyetoka sayari nyingine kabisa. Kwamba inaaminika hakuna Uviko-19, hivyo hapana sababu ya kuogopa.

Nikimtazama Chifu Hangaya, yeye kila siku na kila mahali, anachukua hadhari haachani na barakoa yake mama huyu, lakini sisi Watanzania wengine sijui nini na tumerithishwa na nani, kwamba muda mfupi tu tumejisahau na kuelekea kilele cha mlingoti kwenye joto kali la Uviko-19 ya virusi vipya!

Tunataka nani aje atwambie kuwa Uviko-19 haijaondoka ipo na inaendelea kuua? Tunajisahau.

Wataalamu kwa karama za Mwenyezi Mungu msikatishwe tamaa na Watanzania hawa wabishi na wepesi wa kuyumbishwa na kuachana na utaalamu, endeleeni kuwaasa na kuwanasihi, huenda wakaelewa. Msione mlingoti umepoa katikati mkadhani chini hakuna moto na juu hakuna joto, mwafwa.

UCHUMI

# CRB yakusanya makandarasi wazawa kuwajengea uwezo wawafikie wageni

• Siri yajificha kwenye maarifa na bajeti ya mtaji



Kazi za ujenzi wa barabara kilomita 217, Loliondo hadi Mto wa Mbu, eneo kati ya Wasso hadi Sale (km 49), zilipokuwa zinaendelea Septemba mwaka jana, mkoani Arusha. **PICHA: MTANDAO**

**Na Joseph Mwendapole**

KWA miongo kadhaa kazi kubwa za miradi ya ujenzi wa miundombinu imekuwa ikifanywa na kampuni kubwa za kigeni, huku nchini kukiwapo zaidi ya kampuni 12, 693 zinazokosa uwezo wa kumudu miradi ya nchi.

Ni hali inayotajwa kusababishwa na mambo kadhaa, ikiwamo ukosefu wa mitaji, mitambo na ujuzi wa makandarasi wazalendo kumudu kutekeleza miradi mikubwa kama ya Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP), na Standard Gauge Railways (SGR) inayogharimu trilioni nyingi za fedha za umma.

Kufanikiwa kuwekeza mitaji nyumbani, kunachangia makandarasi wazalendo wanapata nguvu ya kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi kutokana na ukweli kwamba, fedha nyingi zitabaki kwenye mzunguko wa ndani.

Hapo ndipo Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) imeona umuhimu kufikia uamuzi kuwawezesha makandarasi wa ndani, kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo waliko kwenye mikoa mbalimbali nchini.

Ni mafunzo yanayolenga kuwawezesha kupata utaalamu wa kujua mambo ya kufanya wanapojaza fomu za kuomba zabuni, mambo ya kuepuka na namna ya kusimamia miradi ya ujenzi kwa ufanisi.

Kwenye mafunzo yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma, jumla ya makandarasi wa ndani 175 walishiriki mafunzo kuhusu namna ya kutekeleza miradi, kitaalamu inatamkwa "Construction Pre-Contract Practices".

> **"Hii hatua ya kutujengea uwezo ni uamuzi wa kupongezwa kwani kupitia mafunzo haya makandarasi wanapata uzoefu na ujuzi wa kujaza mikataba na kutekeleza.**

Ni mafunzo yaliyotolewa kwa siku na yalilenga kuwasaidia makandarasi hao kuandaa zabuni shindani, ikiwamo mambo yanayopaswa kuzingatiwa katika mchakato mzima kushiriki zabuni. Mambo mengine wamejifunza namna ya kuandaa bei za kazi mbalimbali za ujenzi, ili kuwa na bei shindani za zabuni na hatimaye kuwasilisha zabuni hizo kitaalamu.

Washiriki walielekezwa utumiaji mfumo wa kielektroniki kwenye ununuzi wa miradi ya serikali, TANEPS, unaosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA).

"Mafunzo haya ni muhimu sana kwa kuwa zabuni iliyoandaliwa vizuri, ni lazima hatimaye iwasilishwe ndipo iingie kwenye ushindani. Kwa kuwa Mwajiri mkubwa wa makandarasi ni serikali na serikali inapokea zabuni kupitia TANEPS pekee, basi, umuhimu wa ujuzi wa kutumia TANEPS ni dhahiri mno," anatamka Msajili Msaidizi wa (CRB), Injinia David Jere.

**MWENYEKITI WA BODI**

Mwenyekiti wa CRB, Consolata Ngimbwa, anawaasa makandarasi kuyachukulia umakini mkubwa mafunzo hayo, kwani ndiyo mkombozi wao katika kuongeza ujuzi.

Anasema CRB imejitahidi kuandaa mafunzo mengi, ikiwamo uandaaji mikataba, kujaza zabuni kielektroniki na kuwasilisha zabuni hivyo ni lazima makandarasi wayatumie kuongeza ubora wa kazi zao.

"Kuna mtu anachangia mada kwenye mkutano, lakini akitoka hapo getini yote aliyojifunza anayaacha hapo. Sasa naomba tuyaishi haya tunayojifunza, kwa sababu ni kwa faida yetu sisi wenyewe kukuza biashara hii. Mwezi ujao kutakuwa na mafunzo ya menejimenti na kufanya kazi kwa ubia naomba mhudhurie muongeze ujuzi," anasema

Anasema kazi za ujenzi ziko, ila za ushindani, hivyo, wasibaki kulalamika, bali wayatumie mafunzo kuongeza ujuzi, akisisitiza umakini katika kujaza zabuni kielektroniki na uwekaji bei halisi.

"Hakuna kazi nyingi kwamba kila mtu atapata, lakini zipo za ushindani na ili uweze kushindana kwenye soko hili, ni lazima uwe na ujuzi mkubwa kwenye menejimenti, kujaza zabuni na kusimamia mikataba sasa ukisikia mafunzo njoo yana faida kubwa," anasisitiza.

Anakumbusha serikali imetangaza zabuni nyingi za miradi ya maji na ujenzi wa barabara, hivyo makandarasi wa ndani watakaobahatika kuipata wanapaswa kuitekeleza kwa ufanisi mkubwa.

"Mkifanya vizuri mnajitengenezea njia yenu na ya wengine kuaminiwa, ukifanya vibaya unatuharibia na sisi kuaminiwa. Biashara hii ya ukandarasi ni nzuri tu na ya heshima, kwa hiyo hakikisheni mnalinda heshima ya kazi yetu kwa kufanya kazi nzuri," anasema.

**MKOPO WA MKANDARASI**

Mfuko wa kukopesha makandarasi (Contractors Assistance Fund (CAF), umeandaliwa kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo, huku CRB ikitajwa kwenda mbali zaidi kuanzisha mfuko uitwao CA,F mahsusi kuwakopesha makandarasi wazalendo wanapopata mikataba ya zabuni.

Ni mfuko ambao tayari unatajwa kunufaisha maelfu ya makandarasi wazalendo waliokopa na kufanikiwa kuzirejesha fedha, baada ya kukamilika miradi waliyofanyia kazi.

Msajili Msaidizi wa CRB, Injinia Jere, anasema awali wanachama walikuwa wakikopeshwa kiwango kisichozidi Sh. Milioni 50, lakini sasa umeboreshwa na ukomo wa kukopa umesogea hadi Sh. milioni 100.

Anasema mtaji wa mfuko uliongezeka kutoka Sh Bilioni 3.87 mwaka 2020 mpaka Sh. Bilioni 3.9 mwaka 2021. Pia, idadi ya wanachama wa mfuko imeongezeka kutoka 1,167 mwaka 2020 hadi 1,266 mwaka jana.

"Tunawaomba makandarasi mjiunge na uanachama kwenye mfuko huu kwa sababu mwenye sifa za kukopa ni mwanachama pekee na mtu anapokopa ahakikishe anarejesha fedha ili wanachama wengine waweze kukopa," anasisitiza.

Naibu Msajili huyo wa CRB anafafanua awali mkopo ulitolewa kwa makandarasi wa madaraja kadhaa, lakini sasa unakopesha makandarasi wa madaraja yote, ili mradi mhusika awe mwanachama.

**MAKANDARASI WANENA**

Mkandarasi, Jimy Claudia, mshiriki wa mafunzo hayo, anakumbusha haja ya kuwapo mikakati thabiti inayowawezesha makandarasi wazawa kuhama kutoka ushiriki wa miradi midogo kama ya vyoo na madarasa ya shule.

"Hii hatua ya kutujengea uwezo ni uamuzi wa kupongezwa kwani kupitia mafunzo haya makandarasi wanapata uzoefu na ujuzi wa kujaza mikataba na kutekeleza," anasema

Mwingine, Twikile Joseph, anaungana na mtangulizi wake akijenga hoja:"Tukipata sisi fedha zinabaki kwenye mzunguko wa uchumi hapa hapa nchini, tofauti na wenzetu ambao wengi wanaweka fedha zao nje ya nchi. Hivyo, kikubwa tunachoomba sisi ni serikali kuendelea kutujengea uwezo na nina uhakika tutafika huko waliko wenzetu."



# Serikali yatengea wabunifu bilioni 1/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuendeleza wabunifu watakaoibuliwa kwenye Mashindano ya kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU).

Aidha, hadi sasa wabunifu zaidi ya 480 wamesajili kushiriki mashindano hayo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Aldof Mkenda, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuongezwa kwa muda wa kusajili wabunifu hadi Februari 28, mwaka huu.

Alisema mashindano hayo kitaifa yamepangwa kufanyika jijini Dodoma kuanzia Mei 15 hadi 20, mwaka huu kwa kushirikisha wabunifu kutoka sehemu mbalimbali.

Alisema mashindano hayo ni sehemu ya mikakati ya serikali ya kuongeza hamasa ya matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kama nyenzo ya kutatua kero za kiuchumi na kijamii.

"Mashindano haya ni muhimu sana ndio maana serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuendeleza mashindano hayo katika Wiki ya Ubunifu iliyoandaliwa kwa kushirikiana na programu ya FUNGUO ya UNDP inatarajiwa kufanyika katika mikoa 17 nchini ambayo ni Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Iringa, Mwanza, Zanzibar, Tanga, Kilimanjaro, Morogoro, Njombe, Kagera, Mtwara, Kigoma, Mara na Ruvuma," alisema.

Aidha, Prof. Mkenda alisema kupitia MAKISATU ya mwaka 2019, 2020 na 2021, wizara imefanikiwa kuibua na kutambua wabunifu wachanga 1,785 ambapo kupitia wabunifu hao, bunifu 466 zilikidhi vigezo na zimetambuliwa na kuhakikiwa.

"Kati ya hizo bunifu mahiri 200 tayari zinaendelezwa na serikali ili kufikia hatua ya kubiasharishwa na kati ya bunifu zinazoendelezwa na serikali, 26 zimeshafikia hatua ya kubiasharishwa, huku 95 zikiwa katika hatua ya sampuli kifani na nyingine zipo katika hatua za awali za kuandaa sampuli kifani," alisema.

Alisema Wiki ya Ubunifu na MAKISATU pamoja na mambo mengine, inalenga kuibua, kutambua na kuendeleza jitihada zinazofanywa na wabunifu wa Kitanzania na kuhamasisha matumizi ya sayansi teknolojia na ubunifu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Alieleza kuwa katika mashindano hayo washiriki watashiriki kwenye kutoka makundi saba ambayo ni shule za msingi, shule za sekondari, vyuo vya ufundi stadi, Vyuo vya Ufundi, Vyuo Vikuu, Taasisi za Utafiti na Maendeleo, na mfumo usio rasmi.

Alisema usajili wa ubunifu ulianza Desemba 27, mwaka jana na kwamba umesogezwa hadi Februari 28, mwaka huu, ili kutoa fursa ya watu wengi kushiriki.

# Serikali sasa yataka waajiri kupunguza migogoro ya kazi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Jamal Katundu, amewataka waajiri kuzingatia umri wa ajira pamoja na taratibu za mikataba ya ajira ili kupunguza migogoro mahali pa kazi.

Prof. Katundu alitoa kauli hiyo alipokuwa akifungua kikao cha wadau wa sekta ya habari cha mashauriano kuhusu utekelezaji wa sheria za kazi.

Aidha, alisema ni vyema waajiri waka boresha mahusiano kazini ili wafanyakazi wao wafanye kazi kwa weledi.

Alisema serikali imedhamiria kuwatumikia wananchi kwa kuwapa huduma bora ni vyema waajiri wakaboresha hali ya mahusiano kazini ili kuondoa migogoro.

Kuhusu sekta ya habari, alisema ni vyema waandishi wa habari wakatambua haki zao ikiwamo mikataba ya ajira.

Alisema sekta ya habari ni muhimu katika kuchangia uchumi wa nchi na serikali ina wajibu wa kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji pia wajibu wa kuhakikisha wanalinda haki za wafanyakazi.

Aliwataka wawekezaji kwenye vyombo vya habari wanapoona kuna ulazima wa kuajiri wafanyakazi kutoka nje ya nchi ili kuongeza nguvu katika majukumu yao wasisite kufanya hivyo kwa kufuata taratibu na sheria.

Hata hivyo, Kamishna wa Kazi, Suzana Mkangwa, alisema pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali katika kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi bado kuna kero katika utekelezaji wake.

"Kumekuwa na tabia ya kuwaachisha kazi wafanyakazi bila kufuata taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria pamoja na madai ya mishahara na stahiki zingine za wafanyakazi, hii imesababisha kutokea malalamiko mengi ya baadhi ya wafanyakazi katika sekta muhimu ya habari," alisema.

Naye Mwakilishi kutoka Wizara ya Habari ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Habari Maelezo, Rodney Mbuya, alitaka sekta ya habari kutumia teknolojia kuhakikisha sekta inakuwa zaidi.

Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wafanyakazi, Watafiti, Wanataaluma (RAAWU), Jane Mihanji, alisema kumekuwa na kero kubwa katika kutengeneza ajira za waandishi wa habari ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa vyombo vya Habari Tanzania (JOWUTA), Suleiman Msuya, alisema kero kubwa ya sekta ya habari ni ajira.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Juma Maliki Akil, akimpatia cheti cha ushiriki mafunzo ya kudhibiti ufisadi mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Showalige Mahamoud Ibrahim, yaliyofanyika kwa siku tano jijini Dodoma. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Bunge laitaka wizara vivutio kwa wawekezaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Bajeti imeitaka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuweka vivutio mbalimbali muhimu kwa wawekezaji na kuvifuatilia kama vinatumika ipasavyo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Daniel Sillo, aliyasema hayo juzi katika kikao cha kupokea taarifa kuhusu utaratibu wa utoaji wa vivutio vya kikodi kwa miradi mikubwa ya kimkakati, jijini hapo.

Alisema wizara inatakiwa kuendelea kuweka vivutio hivyo, lakini kuangalia matumizi yake ili kuwa na matokeo chanya kwenye ukuaji wa uchumi wa nchi.

"Tunapendekeza kuboresha uwekaji wa vivutio vya kikodi, uwekaji wa kodi zinazofaa, kuimarisha usimamizi na ufanyaji tathmini kwa vivutio vya kikodi vinavyotolewa, kuangalia kwa makini miradi ya kimkakati inayohitaji kodi, kuongeza muda kwa miradi ya kimkakati iliyobainishwa na kuimarisha ulinzi wa wawekezaji wa ndani," alisema.

Naye Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema serikali itaendelea kuboresha na kuweka mazingira bora ya uwekezaji kwa kuzingatia vivutio vya kikodi.

Aliwahakikishia wajumbe wa kamati hiyo kuyafanyia kazi maoni yote waliyotoa katika kuhamasisha na kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kujenga uchumi endelevu.

Awali Mkurugenzi wa Maendeleo ya Uwekezaji wa Wizara hiyo, Aristides Mbwasi alisema katika utaratibu huo, serikali imefanikiwa kusajili miradi 42 ya wawekezaji mahiri yenye thamani ya Dola za marekani bilioni 12.3.





# JK ahamasisha kuongeza uzalishaji sekta ya kilimo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

RAIS mstaafu Dk. Jakaya Kikwete, amesema serikali inaanzisha programu mbalimbali kwenye sekta ya kilimo ili kuongeza uzalishaji kuhakikisha sekta hiyo inakuwa moja ya sekta muhimu za kuinua uchumi wa Taifa.

Vilevile alisema serikali inalenga kuzitumia programu hizo kuwasaidia wakulima wadogo kuzalisha kwa tija na kuwa na uhakika wa chakula hasa kwa kuzalisha zaidi mazao ya nafaka na mbegu.

Dk. Kikwete ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Shirika la Kuhamasisha Mageuzi ya Kijani Barani Afrika ( AGRA), aliyasema hayo alipofanya ziara ya kikazi katika mikoa ya Mbeya na Songwe kwa ajili ya kukagua miradi.

Miradi aliyokagua ni inayofadhiliwa na Agra katika mikoa hiyo hasa kwenye uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwenye mikoa hiyo kabla ya kuelekea mkoani Rukwa.

"Lengo la serikali kwenye utoaji wa mikopo ya kilimo siyo kuwawezsha wakulima wakubwa na wa kati bali lengo lake ni kuwasaidia wakulima wadogo ili waweze kuinuka kiuchumi, lakini kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini," alisema Dk. Kikwete.

Aidha, aliwataka watafiti wa mbegu za kilimo nchini kuzalisha mbegu bora na zinazoendana na mazingira hususani hali ya hewa ya Tanzania ili kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa tija.

Alisema katika maeneo ambayo alitembelea na kuridhishwa na namna ambavyo mbegu za mazao mbalimbali zinazalishwa na akawataka wananchi kuzitumia mbegu hizo kwenye uzalishaji ili waongeze tija zaidi.

Alisema kabla ya kampuni mbalimbali kuanza kuzalisha mbegu nchini, serikali ilikuwa inatumia fedha nyingi kuagiza mbegu hizo nje ya nchi na kwamba baadhi ya mbegu hizo zilikuwa hazifanyi vizuri kutokana na namna zilivyozalishwa.

Alisema baadhi ya mbegu hizo zilikuwa zinazalishwa kwa ajili ya matumizi ya nchi zinakozalishwa kulingana na hali ya hewa ya huko lakini kwa sasa mbegu nyingi zinazalishwa nchini.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, alisema AGRA imefanya kazi kubwa ya kuwasaidia wakulima wadogo pamoja na wachakataji na kwamba imekugusa kwa kiwango kikubwa na kueleza malengo ya wizara.

"Mpaka sasa AGRA imewasaidia wakulima wadogo wadogo zaidi ya 100,000 na kwamba idadi hiyo itaendelea kuongezeka kutokana na mradi kuendelea kuwapo," alisema Mavunde.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, alisema wawekezaji wa mbegu za mahindi wamekuwa ndiyo wawekezaji wakubwa katika mkoa huo na kudai kuwa mkoa umewapa heka 600 kwa ajili ya kuzalisha mbegu na wamezitumia zote kwenye uzalishaji.

Awali Dk. Kikwete alianza ziara kwa kutembelea Kampuni ya Raphael Group ambayo inajihusisha na uchakataji wa mazao ya nafaka ukiwamo mpunga, karanga, mafuta ya alizeti pamoja na kampuni ya Mbegu ya Meru Company LTD.



Madalali wa kampuni ya Majembe Action Mart Limited wakimwondoa jana mpangaji wa bar maarufu mjini Iringa ya Backyard Lounge baada ya kushindwa kulipa kodi ya Shirika la Nyumba. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Mradi maji waja kumaliza uhaba jijini

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya lita 130 za majisafi na salama zinatarajiwa kuzalishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (UWWSA) baada ya Mamlaka hiyo kwa niaba ya Wizara ya Maji kutia saini mkataba wa ujenzi wa mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Kiwira ulioko wilayani Rungwe ambao ukikamilika utakidhi mahitaji ya maji jijini Mbeya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (CPA), Gilbert Kayange, alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kutia saini mkataba huo ambao hadi sasa serikali kupitia Wizara ya Maji imetoa kiasi cha Sh. bilioni mbili kwa Kampuni ya Lahmeyer Consulting Engineers Ltd ya jijini Dar es Salaam kutekeleza mradi huo.

Alisema mradi huo una lengo la kumaliza kabisa tatizo la maji jijini Mbeya na kwamba kwa sasa wametia saini mkataba na mkandarasi mshauri ili kuanza mradi huo ambapo ataanza utekelezaji wake kuanzia Julai mwaka huu.

"Kwa mwaka 2018 uwezo wa kuzalisha maji kwa mamlaka hiyo ilikuwa ni lita milioni 38.5 ukilinganisha mahitaji ya lita 80 kwa siku, idadi ya watu imekuwa ikiongezeka, kwa kuzingatia umuhimu wa huduma hiyo kwa jamii mamlaka imeendelea kutanua wigo wa huduma na kwamba hadi sasa jumla ya miradi saba inatekelezwa kwa mpigo na kwamba kati ya miradi mitatu tayari imekamilika ambapo wananchi 95,000 wamenufaika," alisema CPA Kayange. Aliongeza kuwa miradi hiyo mitatu baada ya kukamilika imesaidia kuongeza uzalishaji wa lita milioni 13 kwa siku na kusaidia upatikanaji wa lita milioni 51.5 kwa siku hadi sasa

Alisema baada ya kukamilika kwa miradi mingine minne inayoendelea sasa itasaidia kuzalisha lita 15 na kuongeza uzalishaji wa milioni 66 kwa siku.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha sasa huduma za upatikanaji wa maji inakuwa ya uhakika mamlaka imeamua kubuni chanzo cha Mto Kiwira ambacho baada ya kukamilika kwake itasaidia kuzalisha lita 131 kwa siku na kusababisha huduma za maji kwa asilimia 100.

Hafla ya kutiliana saini mkataba huo, ilishuhudiwa na Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, ambaye aliipongeza mamlaka hiyo kubuni chanzo cha Mto Kiwira kumaliza kabisa tatizo la maji jijini Mbeya.

Alisema mradi huo utakamilika kwa miaka miwili kuanzia mwaka 2022 hadi 2024 na kwamba baada ya kukamilika kwake itahudumia wakazi wote wa jiji la Mbeya, lakini huduma hiyo itaweza kusambazwa maeneo mengine kama vile Wilaya ya Chunya, Mbarali na Mkoa wa Songwe.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliiomba Wizara ya Maji kuwasaidia fedha za kukamilisha mradi wa Shongo ambao utahudumia wakazi wa Iyunga na Mbalizi na kusaidia huduma ya maji kupatikana kwa uhakika.

# Vikwazo kwa sekta ndogo ya fedha hivi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MABADILIKO ya mara kwa mara ya viwango vya kimataifa vya usimamizi wa fedha yametajwa kuwa ni miongoni mwa matatizo yanayoikabili sekta ndogo ya fedha nchini.

Mchambuzi wa masuala ya fedha kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Fidelis Mkatte, aliyasema hayo jana wakati akitoa mada kwenye mafunzo ya waandishi wa habari za biashara, uchumi na fedha yanayoendelea jijini Mbeya.

Mkatte alisema kuwa usimamizi wa sekta ndogo ya fedha nchini inapaswa kukidhi viwango vya kimataifa ili Watanzania wasiachwe nyuma katika maendeleo yatokanayo na usimamizi wa fedha. Hata hivyo alisema kuwa sekta ndogo ya fedha nchini inawahusisha Watanzania wenye elimu ya chini na uelewa mdogo hali ambayo inawafanya washindwe kuendana na kasi ya mabadiliko hayo.

"Tunakabiliwa na mabadiliko ya mara kwa mara ya viwango vya usimamizi wa fedha duniani, mabadiliko haya yanapaswa kuingizwa taratibu kwenye jamii yetu kwa vile tunajihusisha na watu wenye uelewa tofauti ambao hawawezi kuendana na kasi ya mabadiliko hayo," alisema Mkate.

Alisema mabadiliko ya viwango vya usimamizi wa fedha yanaendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia duniani, hivyo sekta ndogo ya fedha nchini inalazimika kufanya kila linalowezekana kuendana na mabadiliko hayo.

Aliongeza kuwa mbali na changamoto hiyo, pia kuna changamoto nyingine ya kukosekana kwa uaminifu kwa wafanyakazi wa sekta ya fedha, jambo ambalo linachangia sekta hiyo kuathirika.

Mkate alisema kuwa Benki Kuu ya Tanzania ambayo ndiyo msimamizi mkuu wa sekta ya fedha nchini inajitahidi kukabiliana na changamoto hizo kwa kutoa elimu kwenye jamii.

Meneja wa Idara ya Sarafu wa BoT, Said Ilulu, alisema tatizo kubwa linaloikabili idara hiyo ni utunzaji mbovu wa fedha miongoni mwa wananchi hali ambayo inasababisha uchakavu mkubwa wa fedha.

Alisema Sera ya BoT ni kuhakikisha fedha zinazokuwa kwenye mzunguko ni safi pekee na kwamba zile zinazokuwa zimechakaa huwa zinaondolewa na kuteketezwa kwa utaratibu maalumu.

Aliwataka wananchi kuhakikisha wanazitunza vizuri fedha ili kupunguza gharama za uchapishaji wa fedha hizo huku akisisitiza kuwa baadhi ya wananchi huwa wanaziharibu fedha hizo kulingana na shughuli zao.

"Uchapaji wa fedha ni gharama kubwa, kwa hiyo kinachotakiwa sasa hivi ni wananchi kushirikiana na sisi pamoja na wadau wengine kwenye utunzaji wa fedha ili kuepuka uharibifu huo ambao huwa unafanyika," alisema Ilulu.





# Bodi ya Vileo yapewa neno

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BODI ya Udhibiti Vileo Zanzibar (ZLB), imetakiwa kusimamia Sheria ya Vileo, kama ilivyopitishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kuanza kutumika, baada ya kusainiwa na Rais wa Zanzibar, Mei 11 mwaka 2020.

Wito huo, umetolewa na viongozi wa vyama sita vya siasa Zanzibar ikiwamo CHADEMA, AAFP, DP, ADA-TADEA na NLD, walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari kwa nyakati tofauti, kuhusu utekelezaji wa sheria hiyo.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee CHADEMA, Hashimu Issa Juma, alisema jambo la faraja ni kuona Bodi ya Vileo, ikianza kazi vizuri baada ya Rais Dk. Hussein Mwinyi, kuvunja bodi ya zamani na kuuuda mpya, kutokana na kushindwa kusimamia Sheria Namba 9 ya Vileo ya Mwaka 2020.

Hashimu alisema hatua ya bodi kuteua kampuni tatu kati ya tisa, zilizojitokeza katika zabuni ya mwaka 2022, kumezingatia masharti ya kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Udhibiti Vileo, baada ya muda mrefu kukiukwa, tangu ilipoanza kutumika baada ya rais kusaini.

"Rais Dk. Hussen Ali Mwinyi, anastahili kupongezwa kwa hatua alizochukia. Tumeshuhudia bodi ya vileo ikiondoa utitiri wa kampuni za kuingiza vileo Zanzibar, hatua hii itasaidia pia kudhibiti biashara za vileo za magendo," alisema Hashimu.

Alisema, kwa mujibu wa masharti ya Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Vileo ya Vibali vya Uingizaji Vileo, hutolewa kwa kampuni tatu na wamiliki wa kampuni lazima wawe Wazanzibar.

Mwenyekiti wa AAFP, Said Soud Said, alisema bodi inapaswa kuendelea kufanya ukaguzi kwenye baa, ambazo zinalalamikiwa kuwa kero zilizopo katika maeneo ya huduma za jamii, kama vile nyumba za ibada, shule, hospitali na makazi ya watu kinyume na masharti ya Kifungu cha 28(k) cha Sheria ya Vileo Namba 9 ya Mwaka 2020.

Aidha, alisema kampuni zilizokosa zabuni ya uingizaji wa vileo mwaka 2022, zinapaswa kuheshimu maamuzi ya Bodi ya Vileo, ili malengo ya serikali ya kutunga sheria mpya yaweze kufikiwa kwa maslahi ya nchi na wananchi wa Zanzibar.

"Vitendo vya udhalilishaji wanawake na watoto vimekuwa vikiongezeka Zanzibar, kutokana na kuongezeka biashara ya vileo katika makazi ya watu na kuvuruga mila na utamaduni wa Zanzibar," alisema Soud.

Mwenyekiti wa NLD, Mfaume Khamis, alisema Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wanapaswa kupongezwa kwa kupitisha sheria mpya ya bodi hiyo na sasa matunda yameanza kuonekana baada ya kuundwa mpya.

"Tangu sheria hiyo ipitishwe mwaka 2020, ilikuwa haifanyikazi bila watendaji kuchukuliwa hatua. Kwa kweli hatuna budi kumpongeza rais kwa kuvunja bodi na kuunda mpya. Sheria itabaki kuwa msumeno na kutenda haki, " alisema Mfaume.

Makamu Mwenyekiti wa DP, Peter Magwira, alisema udhibiti wa biashara ya vileo katika maeneo ya huduma jamii na makazi ya watu kutasadia kulinda mila na utamaduni wa Zanzibar.

Hata hivyo alisema vyombo vya ulinzi na usalama kikiwamo Kikosi cha Kuzuia Magendo, Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), zinapaswa kushirikiana ili kulinda mapato ya serikali na kudhibiti vileo vinavyoingizwa kwa magendo Zanzibar.

Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadir Abdulratifu, alisema lengo la kutungwa sheria mpya ya vileo ni kupunguza utitiri wa baa katika makazi ya watu na huduma za jamii pamoja na kudhibiti biashara za magendo.

"Bodi ya Udhibiti wa Vileo, imeanza kuchapakazi vizuri hivyo tunawatahadharisha huko tuendako siku za usoni wasije kugeuka na kufanya mambo kinyume cha sheria," alisema Nadiri.

Naibu Katibu Mkuu wa AD- TADEA, Rashid Yussuf Mchenga, alisema usimamizi mzuri wa sheria utasaidia kuimarisha misingi ya demokrasia na utawala bora visiwani humo.

# Bandari kavu sasa kujengwa Mpigaduri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji, Rahma Kassim Ali, amesema eneo la Mpigaduri lililoko Maruhubi, Unguja, litajengwa bandari kavu kwa lengo la kupunguza msongamano katika Bandari ya Malindi Unguja.

Waziri huyo aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, Machano Othman Said, akitaka kujua hatima ya Bandari ya Malindi, ambayo imezidiwa na msongamano wa makontena na kuzorotesha shughuli katika bandari hiyo.

Alikiri kwamba, Bandari ya Malindi imezidiwa na msongamano mkubwa wa shughuli mbalimbali, ikiwamo kazi za kutoa huduma za abiria wanaosafiri kati ya Tanzania Bara na Pemba.

Alisema serikali imechukuwa uamuzi wa kufanya eneo la Mpigaduri kutumika kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu, ambayo itahifadhi makontena na mizigo.

Alifafanua kwamba, kazi inayofanywa kwa sasa ni upembuzi yakinifu ikiwamo michoro ya ujenzi wa bandari hiyo, ambayo itasaidia kupunguza msongamano mkubwa wa makontena yalioko katika Bandari ya Malindi.

Aidha, alisema Bandari ya Malindi inakusudiwa kugeuzwa kuwa bandari ya utalii, kutokana na kuwapo katika eneo la Mji Mkongwe wa Zanzibar, ambao umeingizwa katika urithi wa mambo ya kale wa kimataifa.

Alisema serikali inaendelea na mipango yake ya kujenga bandari kubwa ya kisasa ya Mangapwani Wilaya ya Kaskazini Unguja, ambayo itahusisha pia huduma za bandari nyingine, ikiwamo za uvuvi, makontena na chelezo ya kutengeneza na kufanyia matengenezo meli na boti. "Hiyo ndiyo mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuona kwamba tunajenga bandari kubwa ya Mangapwani, Unguja, ambayo itahusisha bandari nyingine, lakini Bandari ya Malindi itatumika kwa ajili ya shughuli za usafiri na watalii," alisema.

Hata hivyo, alibainisha mipango ya serikali kuendelea kujenga bandari nyingine Kizimkazi, Shumba mjini, Wete pamoja na Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini, ambayo kwa sasa ipo katika hatua ya gati.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Magonjwa yasioambukiza bado yapewa kipaumbele'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema maradhi yasiyoambukiza ikiwamo kisukari na shinikizo la damu, yamepewa kipaumbele kuhakikisha huduma za matibabu yake, yanapatikana.

Waziri wa wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Zawadi Amour Nassor, aliyetaka kufahamu mikakati ya wizara katika kutoa huduma za afya kwa maradhi yasiyoambukiza ikiwamo kisukari na shinikizo la damu.

Alisema tayari jumla ya vituo 53 vimeanzishwa kwa ajili ya kutoa huduma za matibabu kwa maradhi yasiyoambukiza, huku upande wa Unguja ni vituo 34 na Pemba 19.

Alisema zaidi ya watu 60,000 wanasumbuliwa na maradhi ya kisukari nchini na kwamba athari zake kwa afya ya binadamu ni kubwa ikiwamo kupata ulemavu wa kudumu.

"Mheshimiwa Naibu Spika nataka niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imejipanga kupambana na maradhi yasiyoambukiza kisukari na shinikizo la damu," alisema.

Mazrui aliwataka wananchi kutumia dawa za hospitalini, ambazo zimefanyiwa vipimo vinavyokubalika kiafya na kuwataka kuacha kutumia dawa za miti shamba.

Alibainisha kwamba, dawa za miti shamba husababisha athari kubwa kiafya ikiwamo kuathiri baadhi ya viungo muhimu vya mwili kama vile figo kushindwa kufanya kazi vizuri.

"Wizara ya Afya, inawataka wagonjwa wanaosumbuliwa na maradhi ya kisukari kutumia dawa rasmi zinazotolewa katika vituo vya afya na kuacha kutumia dawa za miti shamba, ambazo hazina vipimo vinavyokubalika kitaalamu," alisema Mazrui.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi na 280/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU hamisi salumu wa MZENGELA**
**KATIKA SHAURI KA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA mwanahamisi shabani matatilo**

**TANGAZO**

(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 mwezi 02 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 8 mwezi 2 mwaka 2022

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**Wilaya ya TANGA Kituo cha Mjini Tanga**
**Mkoa wa Tanga**
**Usimamizi wa mirathi namba 29/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HAMMOUD SALIM AMRI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MOHAMED SALIM AMRI**

**TANGAZO**
[Kanuni ya 5[2] ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo]

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24 mwezi 2 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kua msimamizi wa mirathi hiyo.
Imetolewa tarehe 14 mwezi 02 mwaka 2022

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi Na.05/2022**

**Jesta Joel Mwinami……………Marehemu**
**Augustono Nyagawa………………….Msimamizi**

**TAARIFA KWA UMMA**
KUTANGAZA MAOMBI YA KUFUNGA MIRATHI
Kwa wanaodai kuwa na haki na marehemu aliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika katika Mahakama hii na kuangalia orodha ya mali za marehemu [fomu namba V] na hesabu za mirathi [fomu namba VI] katika jalada la mirathi.
Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali [ fomu namba V] na au hesabu za mirathi [fomu namba VI] hii yawe yameandikishwa katika mahakama hii mnamo au kabla ya siku ya tarehe 16th ya mwezi wa March mwaka 2022 mpaka kufikia saa 9:30 alasiri
Imetolewa na Hakimu mkazi leo siku ya **tarehe 16th februari mwaka 2022.**

---

**TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA BAJAJ**

**MAGRETH DIONIS MJINDO ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya BAJAJ yenye namba za usajili MC 318 CLM Injini namba AK4NK4801623 chasiss namba MD6M14PA2K4NO1612 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/61116/2022**

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**RAJABU JUMA MANGARA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MAZDA DEMIO lenye namba za usajili T 346 CMF ,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi**
**Polisi taarifa DAR/URA/RB/70518/2022**

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI NAMBA: 12/2021**
**MDAI: ULUGURU PHAMACETICAL NA ASSOCIATE COMPANY**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: BURE HAMISI SALEHE, HAMISI HAMISI MANULA, RAMLA AMRI, MSAJIGWA MWAKILUMA, LEONARD MASATU**
**KWA: 1.HAMISI HAMISI MANULA**
**2. RAMLA AMRI**

**POPOTE MULIPO**
Mahakama hii inakufahamisha kwamba mdai amefungua shauri la madai tajwa hapo katika mahakama hii.
Hivyo shauri limepangwa kutajwa mnamo tarehe 02/03/2022 saa 2.30 asubuhi na mnatakiwa kuwepo, a kuwasilisha kisheria pamoja na kuleta utetezi wako dhidi ya madai haya.
Zingatia kwamba kutofika kwako tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila yaw ewe kutaarifiwa tena, na mamuzi kutolewa.
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 16 Mwezi 02 Mwaka 2022.

**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MAHAKA MA YA WILAYA**
**MOROGORO**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya**
**Wilaya ya Morogoro mjini**
**Kituo cha Kihonda Mkoa Morogoro**
**Shauri la ndoa Na. 04…2022**
**Jina la mdai: Valentina Benedict**
**Jina la mdaiwa Laurent:Saimon Mahengeta**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama ya Mwanzo)

Kwa Laurent simon Mahengeta Modeko "A"
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake Kwamba (Elezea hapa habari za madai) Madai ya kuomba ndoa ivunjwe na mgawanyo wa mali.
Kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 23 Mwezi 2 Mwak 2022 saa 2 Asubuhi / Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwajili kujitetea.
ANGALIZO:Kama hautohudhiria siku iliyo tajwa hapo juu na ikathibitika kuwa ulipkea hati ya kuitwa shuarini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 17 Mwezi 02 Mwaka 2022

---

**TANGAZO LA KUPOTEA KWA CHETI CHA USAJIRI WA KAMPUNI**

**TANZANIA HOME ECONOMICS ASSOCIATION (TAHEA) inatangaza kupoteza cheti cha usajiri chenye namba SO. 6179 (IMEWEKWA KUSIKOJULIKANA) Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba DOD/DOD/RB56990//2022**

---

**TANGAZO LA KUPOTEA KWA CERTIFICATE OF COMPLIANCE**

**TANZANIA HOME ECONOMICS ASSOCIATION (TAHEA) No. 1732 (IMEWEKWA KUSIKOJULIKANA) Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/69861/2022**

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Viongozi EU watilia shaka ishara Russia kuondosha majeshi yake

**MOSCOW,** URUSI

VIONGOZI wa Ulaya, wanasema hakuna ishara zozote kuonyesha Urusi inaondosha wanajeshi wake kutoka mipaka ya Ukraine, huku Rais Joe Biden wa Marekani, akionya kwamba iko tayari kujibu vikali.

Juzi, Moscow ilitangaza kwamba inaanza kuondoa sehemu ya wanajeshi na vifaa vyake vya kijeshi baada ya kukamilisha zoezi kubwa, nchini Belarus na jana kutangaza kukamilisha mazoezi kwenye peninsula ya Crimea.

Katibu Mkuu wa Muungano wa NATO, Jens Stoltenberg, akizungumza kabla ya mkutano na mawaziri wa ulinzi alisema wako tayari kwa hali yoyote itakayojitokeza na Urusi itakumbwa na hasara kubwa ikithubutu kuivamia Ukraine.

Katibu mkuu wa NATO anaeleza: Tutaendelea kupeleka ujumbe ulio wazi kabisa kwa Urusi, kwamba sisi tuko tayari kukaa chini kwa mazungumzo pamoja nao. Lakini wakati huo huo, tuko tayari kukabiliana na hali yoyote mbaya itakayotokea."

Wito kama huo, ulitolewa pia na Kamishna wa Umoja wa Ulaya, Ursula Von Der Leyen alipokuwa analihutubia bunge la Umoja wa Ulaya juzi, Jumatano.

Der Leyen, alieleza: Umoja wa Ulaya na washirika wetu upande wa pili wa Atlantiki tumeungana katika kukabiliana na mzozo huu na wito wetu kwa Russia ni bayana kabisa isichague vita.

"Njia ya ushirikiano kati ya Urusi na sisi inaweza kufanyika. Lakini tubaki makini. NATO haijaona bado dalili za kupunguzwa kwa wanajeshi wa Urusi."

Juzi, wizara ya Ulinzi ya Russia ilitangaza kwamba inaondoa baadhi ya wanajeshi wake na vifaa vya kijeshi kutoka Belarus baada ya kukamilisha zoezi la kijeshi. Na hii leo imetoa video nyingine ikionyesha kuondolewa kwa vifaa vyake kutoka peninsula inayoikalia ya Crimea.

Akiwahutubia wamarekani kwa mara ya kwanza tangu kuzuka kwa mvutano huo Rais Joe Biden alisisitiza kwamba hakuna mabadiliko kwenye mpaka kati ya Urusi na Ukraine na hawawezi kuthibitisha bado kwamba wanajeshi 150,000 wameanza kuondolewa.

Rais Biden, alieleza: Ikiwa Urusi itaendelea na mipango yake, tutaungana pamoja kupinga uvamizi wake, Marekani na washirika wake kote duniani wako tayari kuiwekea vikwazo vikali dhidi ya bidhaa zake zinazosafirishwa nje, pamoja na hatua nyinginezo, hatukufanya chochote ilipovamia mashariki mwa Ukraine 2014. **DW**

# Washangaa wabunge kudai kununuliwa makoti ya mvua

**Lilongwe,** MALAWI

WANANCHI wa Malawi, wanawakosoa wabunge wao baada ya mbunge kuliomba bunge kuwanunulia makoti ya mvua.

Mbunge wa Lilongwe Kusini, Steven Kamsiyamo alitoa ombi hilo juzi, akisema walihitaji kujikinga na mvua wakati wakitembea hadi ndani kutoka eneo la maegesho ya magari.

Inasemekana kwamba kiongozi huyo wa bunge aliwahakikishia wabunge kuwa suala hilo litapelekwa kwa kamati ya tume ya bunge, ili kuzingatiwa.

**Tuna waathiriwa wa mafuriko huko Salima na Lower Shire ambao wanahitaji msaada.**

Baadhi ya Wamalawi, wamekasirishwa na hatua hiyo wakisema wabunge hao walikuwa wabinafsi na wasio na hisia, wakati mafuriko yameharibu familia nyingi kote nchini.

"Tuna waathiriwa wa mafuriko huko Salima na Lower Shire ambao wanahitaji msaada. Kwa nini upoteze pesa kwenye makoti ya mvua?" Bright Malenga aliuliza kwenye Twitter.

"Kiwango hiki cha haki hakiwezi kufikirika," mtumiaji mwingine wa Twitter alisema.

Mafuriko yaliyosababishwa na kimbunga Ana, yaliua makumi ya watu na kuharibu mashamba, nyumba na barabara.

Wiki iliyopita, mamlaka ya hali ya hewa, ilitoa tahadhari ya mafuriko katika maeneo ya kati na Kaskazini mwa Malawi. **BBC**



Mbwa akiokolewa na mwokoaji baada ya kukwama kwenye tope lililotokana na maporomoko ya udongo katika makazi ya watu jijini Petropolis, nchini Brazil jana, inakadiriwa watu 100 wamepoteza maisha. **PICHA: AP**

# Maporomoko ya ardhi yaua 100 Brazil

**PETROPOLIS,** BRAZIL

TAKRIBANI watu 100 wamefariki kutokana na maporomoko ya ardhi na mafuriko katika mji wa Petropolis nchini Brazil, maofisa wamesema.

Jiji hilo, ambalo liko kwenye milima Kaskazini mwa Rio de Janeiro, lilikumbwa na mvua kubwa.

Nyumba katika vitongoji vya milimani ziliharibiwa na magari kusombwa na maji, huku mafuriko yakipita katika mitaa ya jiji hilo.

Timu za utafutaji na uokoaji zinakabiliana na tope kutafuta walionusurika.

Jeshi la Ulinzi la Kitaifa la Brazil, lilisema kwenye Twitter watu 24 wameokolewa wakiwa hai hadi sasa na vifo 94 vilivyothibitishwa.

Video zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha uharibifu mkubwa na magari yakielea mitaani.

"Hali inakaribia kama vita. Magari yanayoning'inia kwenye nguzo, magari yamepinduka, matope mengi na maji bado yapo," Gavana wa Rio de Janeiro Claudio Castro aliwaambia waandishi wa habari. **BBC**

# AU, EU wajadili ushirikano Brussels

**BRUSELLS,** UBELGIJI

VIONGOZI wa Umoja wa Afrika (AU) na wa Umoja wa Ulaya (EU), wamekutana mjini Brussels kwa mazungumzo ya siku mbili kuanzia jana.

Wanalenga kuimarisha ushirikiano, huku Ulaya ikiahidi uwekezaji mkubwa barani Afrika, inakokabiliwa na ushindani wa China na Urusi.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkuu wa Diplomasia wa Umoja wa Ulaya, Josep Borrel, alisema Ulaya inapaswa kuisaidia Afrika kuyashughulikia matatizo yake.

Uhusiano baina ya mabara hayo mawili, umekuwa ukitiwa doa na mlolongo wa matatizo, yakiwamo usambazaji wa chanjo ya Covid-19, namna ya kuzuia uhamiaji haramu, wimbi la mapinduzi ya kijeshi barani Afrika na ushawishi wa mamluki wa Urusi barani humo.

Rais wa Senegal, Macky Sall ambaye ni Mwenyekiti wa AU, alisema lengo la mkutano huo ni kufikia uhusiano mpya unaodhihirika kwa vitendo. **DW**

# TANGA WAITAKA FAINALI KOMBE LA FA 'ASFC 2022'

**Na Bakari Cheji,** TANGA

CHAMA cha Soka Mkoa wa Tanga (TRFA), kimeandika barua katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kuomba wenyeji wa mechi ya hatua ya nusu fainali au fainali ya mashindano ya Kombe la FA (ASFC) ili ichezwe kwenye Uwanja wa CCM Mkwakani jijini hapa, imefahamika.

TRFA imefanya uamuzi huo baada ya kupokea pia maoni kutoka kwa wadau wa soka wa jijini hapa. Ombi hilo limekuja baada ya michezo ya hatua ya 16 bora kumalizika juzi ambapo tayari timu nane zimefuzu kucheza hatua ya robo fainali ikiwamo Coastal Union.

Timu nyingine zilizofika hatua ya robo fainali ni pamoja na mabingwa watetezi, Simba, Yanga, Azam FC, Kagera Sugar, Polisi Tanzania, Geita Gold FC na klabu pekee inayoshiriki Ligi ya Championship, Pamba ya jijini Mwanza.

Akizungumza na Mwakilishi wa Vilabu wa Tanga, Martin Kibua, alisema kikao cha Kamati ya Utendaji ya TRFA kilichokutana Desemba mwaka jana kilifanya uamuzi wa kuiandikia barua TFF kuomba moja kati ya mechi hizo ili kuwapa mashabiki wa jijini hapa burudani.

**"Mwaka jana Kamati ya Utendaji ya TRFA chini ya Mwenyekiti, Said Soud tulikutana na kujadili barua iliyoandikwa na TFF ka tika mikoa kupeleka maombi ya kucheza fainali au nusu fainali ya Kombe la FA, lakini bado hatujapata majibu ila tunaioba TFF itupatie mojawapo kati ya nafasi hizo mbili," alisema Kibua.**

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Hamasa ya Coastal Union, Salim Bawazir, amesisitiza wanaoomba TFF iwapatie nafasi mojawapo kwa sababu Tanga ni mkoa wa kimichezo na kuna amani, usalama na hoteli za kutosha za kuwahifadhi wageni watakaokuja.

Meneja wa Uwanja wa CCM Mkwakwani, Nassoro Makau, kwa upande wake alisema uwanja huo upo katika hali nzuri na tayari kutumika kwa mechi mojawapo kati ya hizo walizoomba.

Makau alisema changamoto ndogo ndogo ambazo zipo zinaendelea kurekebishwa kwa ajili ya kufikia viwango vinavyotakiwa.

"Mimi meneja wa Mkwakwani na mdau wa soka nasema tupo tayari na tunahitaji mojawapo kati ya mechi hizo zichezwe hapa kutokana na uwanja unaridhisha," Makau alisema.

Mechi za hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo mwaka jana zilichezwa katika viwanja viwili vya Majimaji, Songea mkoani Ruvuma na Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora huku fainali ikipigwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma na kushuhudia Simba ikitetea ubingwa wake kwa kuwafunga Yanga bao 1-0.

# Pamba yaanika siri ya ushindi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Pamba FC ya Mwanza, Willbert Mweta, amesema walitumia siku tatu kuisoma Dodoma Jiji na baada ya kujua mfumo wanaopenda kuucheza, wakatengeneza mpango mkakati uliowasaidia kupata ushindi katika mchezo wao wa hatua ya 16 bora wa Kombe la FA uliochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagama jijini Mwanza juzi.

Pamba ilisonga mbele kwa ushindi wa mabao 2-1, na kuwa timu pekee ya madaraja ya chini iliyotinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Mweta alisema baada ya kugundua Dodoma Jiji inapenda kushambulia kwa kutumia mabeki wa pembeni na kuwaacha walinzi wawili, wao walitengeneza mfumo wa kukaa nyuma na kushambulia kwa kushtukiza kwenye maeneo ambao mabeki wao hawapo, kitu ambacho kiliwasaidia katika mechi hiyo.

Kocha huyo pia aliwashukuru wachezaji wa timu hiyo, mashabiki wa viongozi kwa kuungana na kuwa kiti kimoja na hatimaye kufika hatua hiyo kwenye michuano hiyo ambayo bingwa hupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mabao ya Pamba yalifungwa na Makiada Makolo na Malulu Masunga huku lile pekee la Dodoma Jiji likipachikwa wavuni na Cleophace Mkandala.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Aisha Juma (kulia), akipambana kuwania mpira na mchezaji wa Fountain Gate Princess katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mo Arena jijini Dar es Salaam juzi. Simba Queens ilishinda mabao 3-1. **PICHA: SIMBA SC**

## Kipigo cha Simba chamtesa Masau

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushushiwa gharika ya mabao 7-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kutoka kwa mabingwa watetezi wa michuano ya Kombe la FA, Simba, Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, ametaja sababu tatu zilizosababisha timu yake kupata kichapo hicho.

Alitaja sababu mojawapo ni wachezaji wake bado walikuwa kwenye majozi ya msiba wa mwezao, aliyefariki hivi karibuni, Ally Mtoni 'Sonso'.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Masau alisema ilikuwa si usiku mbaya, ambapo kila Mtanzania alishangazwa na matokeo hayo na kuongeza hayakuwa rafiki kwa afya za mashabiki na wapenzi wa Ruvu Shooting.

"Matokeo si rafiki kwa afya zetu sisi viongozi, mashabiki wa wachezaji wa Ruvu Shooting, lakini naweza kusema sababu tatu ambazo zimesababisha kipigo hicho," alisema Masau.

Alitaja sababu nyingine ni wachezaji wao kuonekana kuidharau Simba hali wanafahamu ina wachezaji wazoefu na walio na uchu wa kufunga.

"Tatu ni suala na majira, wakati na ukombozi. Atakayetafakari, atajua nini naongea kuhusu hili," Masau aliongeza.

## Kiduku aingia kambini kujifua

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa hapa nchini, Twaha Kiduku, ameingia kambini rasmi kwa ajili ya kujiandaa na pambano dhidi ya mpinzani wake, Alex Kabangu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), litakalofanyika Machi 26, mwaka huu mkoani Morogoro.

Pambano hilo lisilokuwa na ubingwa litakuwa la raundi 10 na la uzito wa Super Middle.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kiduku alisema Kabangu ni bondia mzuri hivyo anapaswa kujiimarisha na kuingia ulingoni kwa tahadhari.

"Kabangu ni bondia mzuri, nimemfuatilia mapambano yake mbalimbali aliyowahi kucheza hapa nchini, hivyo lazima niingie kwa tahadhari kwa sababu ninahitaji kubakisha mkanda," alisema Kiduku.

Aliongeza anajifua kuhakikisha hawaangushi Watanzania katika pambano hilo kwa kumpiga mpinzani wake mapema ingawa amejiandaa kukutana na ushindani.

Mara ya mwisho Kiduku kupanda ulingoni ilikuwa ni Agosti 20, mwaka jana, kwa kupambana na Abdallah Pazi maarufu Dulla Mbabe ambapo aliibuka mshindi na kuondoka na zawadi ya gari.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### POGBA KUONDOKA UNITED

KIUNGO wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28 yuko tayari kupokea ofa kutoka klabu nyingine za Ligi Kuu England wakati mkataba wake na Manchester United utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. (***Telegraph***)

#### EZE ANUKIA NEWCASTLE

NEWCASTLE inajiandaa kutoa ofa ya pauni milioni 45 kwa ajili ya kiungo mchezeshaji wa Crystal Palace, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 23. (***Mirror***)

#### LINGARD AIKATAA SPURS

NYOTA wa Manchester United, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29 anaweza kukacha kuhamia Tottenham Hotspur bure mwishoni mwa msimu. Kiungo huyo mshambuliaji wa England angetamani kucheza nje ya nchi hiyo (***Express***).

#### NDOMBELE KUBAKI LYON

RAIS wa Lyon, Jean-Michel Aulas amegusia klabu hiyo huenda ikamsajili moja kwa moja kutoka kwenye mkopo kiungo Mfaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 25 akitokea Tottenham Hotspur kama timu hiyo itatwaa Kombe la Ligi ya Europa. (***RMC Sport, via Standard***).

#### RAPHINHA SAFARI IMEIVA

WINGA wa Brazil na Leeds United, Raphinha mwenye umri wa miaka 25 ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool, amekataa kusaini mkataba mpya wa kubakia katika klabu yake hiyo ya Elland Road. (***Liverpool Echo***)

#### WILLIAMS AREJESHWA UNITED

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ralf Rangnick amefanya "usajili" wake wa kwanza kwa kumfahamisha mlinzi wa pembeni, Brandon Williams mwenye umri wa miaka 21, kwamba atarejea Old Trafford mkataba wake wa mkopo utakapomalizika pale Norwich. (***Sun***)

#### UNITED KUMBANA RANGNICK

KLABU ya Manchester United huenda ikazuia tena mahitaji hayo ya uhamisho ya Ralf Rangnick baada ya kufanya hivyo Januari kwa kiungo Mfaransa wa RB Leipzig, Christopher Nkunku, mwenye umri wamiaka 17. (***Bild, via Express***)

#### ARSENAL YAMTAKA LEAO

ARSENAL ni timu ya hivi karibuni ya Ligi Kuu England iliyoonyesha nia ya kumtaka mshambuliaji wa AC Milan, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 22. (***La Repubblica, via Metro***)

#### SCHAR ATAKIWA SEVILLA

KLABU ya Newcastle inakabiliwa na mtihani wa kumbakiza mlinzi wake kutoka Uswisi, Fabian Schar mwenye umri wa miaka 30 ambaye mkataba wake wa mkopo unaelekea ukingoni kule AC Milan, huku Sevilla na Valencia zikimtaka. (***Mail***)

#### RODGERS : NDIDI BEI KUBWA

KOCHA Brendan Rodgers amesema nyota wa Leicester City, Wilfred Ndidi "ana thamani kubwa" zaidi ya pauni milioni 50 baada ya Aston Villa kuhusishwa na kiungo huyo raia wa Nigeria mwenye umri wa miaka 25. (***Birmingham Mail***)

#### ANTHONY KUONDOKA AJAX

KLABU ya Manchester United inavutiwa kumsajili winga Ajax, Antony mwenye umri wa miaka 21 ambaye huenda akaungana na kocha Erik ten Hag pale Old Trafford kama uhamisho huo utazaa matunda. (***90min, via Express***)

## DONDOO ZA SOKA
### MAGAZETI YA ULAYA



# USAJILI SPURS WAMKERA CONTE

### ●●● Asema wazi hajafurahishwa na mchakato uliofanywa katika dirisha la...

**LONDON,** ENGLAND

ANTONIO Conte haonekani kufurahishwa kupita kiasi na biashara ya Tottenham katika dirisha la usajili la Januari ambalo lilisajili wachezaji wawili pekee.

Conte alikuwa ameweka wazi nia yake ya kuongeza wigo wa kikosi kinachofukuzia kumaliza katika nafasi nne za juu kwenye Ligi Kuu England.

Tanguy Ndombele, Bryan Gil na Giovani Lo Celso walitolewa kwa mkopo huku Dele Alli akiondoka kabisa.

Lakini badala ya wachezaji wanne wa kikosi cha kwanza, ni wawili pekee waliofika kwenye kikosi ambao ni nyota wa Juventus, Dejan Kulusevski na Rodrigo Bentancur.

Spurs walikuwa wakihusishwa kutaka kuwanunua Adama Traore na Luis Diaz, lakini badala yake nyota hao wakajiunga Barcelona na Liverpool.

Na Conte, aliyeteuliwa mnamo Novemba, mwaka jana alidokeza kutoridhika kwake katika mahojiano na Sky Sport.

**"Kilichotokea Januari sio rahisi," alisema. "Wachezaji wawili tu waliwasili.**

"Kwa hiyo hata kwa namba, badala ya kuimarisha, unaweza kuwa nao kwenye karatasi, dhaifu."

Conte, ambaye ameshinda mataji matano ya ligi kwa muda wote akiwa na Juventus, Chelsea na Inter, pia aliangazia wasifu wa wachezaji hao wawili wapya.

Kulusevski ana umri wa miaka 21 na alikuwa ameanza mechi tano pekee za Serie A msimu huu, huku Bentancur, akiwa na umri wa miaka 24, alihusika zaidi na Juve kwa mechi 13 alizocheza.

"Bentancur na Kulusevski ndio matarajio bora kwa Tottenham," Conte alisema, "kwa sababu Tottenham inatafuta wachezaji wachanga, wachezaji wa kuendelezwa, sio wachezaji walio tayari."

Alipoulizwa maoni yake juu ya mbinu hii, kocha huyo aliongeza: "Ni lazima ukitaka kukua kwa kasi na ukitaka kuwa na ushindani wa haraka, unahitaji wachezaji wenye uzoefu mkubwa, kwa sababu wanaongoza kuongeza uzoefu pia katika timu yako.

"Lakini basi tena, maono ya klabu, naelewa mambo yalikuwa magumu."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 940

MECHI KALI
JUVENTUS
VERSUS
TORINO
1 | 1.66
X | 3.71
2 | 5.33

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# POGBA YUKO NJIA MOJA



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United wanakabiliwa na uwezekano wa kumpoteza kiungo wao, Paul Pogba kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa yuko katika miezi minne ya mwisho ya mkataba wake uliopo na kuna dalili chache kwamba yuko tayari kuongeza muda wake hapo Old Trafford.

Na katika pigo zaidi kwa United, wanaweza kumshuhudia Pogba akielekea kwa mmoja wa wapinzani wao wa Ligi Kuu England.

Gazeti la Telegraph limeripoti Pogba, ambaye alijiunga tena na United kutoka Juventus kwa dili la fedha nyingi mwaka 2016, yuko tayari kusubiri hadi mwisho wa msimu ndipo aamue mustakabali wake.

Kusaini mkataba mpya na United bado inaonekana kuwa ngumu, lakini Pogba hatakuwa na chaguo iwapo atapatikana akiwa huru.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 atazipima klabu nyingine za Ligi Kuu England zinazomwania, huku Chelsea na Manchester City zikiwa zimehusishwa hapo awali.



# Klopp: Tumeshinda lakini haikuwa siku nzuri kwetu

**MILAN,** Italia

JURGEN Klopp alipongeza "uchezaji wa kiutu uzima" kutoka kwa Liverpool baada ya ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Inter kwenye Uwanja wa SanSiro, juzi Jumatano.

Wekundu hao wa Anfield hawakuwa na kiwango bora zaidi katika mechi hiyo ya kwanza ya hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini bado walipata faida ya mabao ya dakika za lala salama kutoka kwa Roberto Firmino na Mohamed Salah.

Klopp alifurahi kuona timu yake ikithibitisha kwa mara nyingine inaweza kupata matokeo kwenye michezo ambayo inaonekana kuwa ni migumu kwao.

Aliiambia BT Sport; "Ilitubidi tupam-
bane. Tulianza vizuri sana, tuliche
karibu na mfumo wao mwanzo, lak
mchezo wa moja kwa moja wa ku
adilisha mabeki wa pembeni hatul
linda vizuri.

"Mara nyingi mabeki wetu wa pe
beni walikuwa peke yao katika hali
mtu mmoja mmoja, haifanyi kazi ip
avyo hivyo.

"Katika mchezo kama huu lazin
uwe na mpira kwa muda mrefu na h
halikufanyika kwa muda wa kutosha

"Lakini huwezi kuja hapa na ku
maini kuwa una siku nzuri na hi
ndiyo nafasi pekee ya kupata matoke

"Hatukuwa na siku nzuri, lakini si
nzuri ya kutosha kuwa ushindi unad
tahili. Tulifunga mabao mawili ya a
bu, ndiyo walikuwa na wakati wao
mashambulizi ya kushtukiza.

## HABARI MICHEZO

,850,660

# MAJALIWA MGENI RASMI KILIMANJARO MARATHON

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya miaka 20 ya mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon zitakazofanyika Februari 27, mwaka huu Moshi, mkoani Kilimanjaro.

**Majaliwa anatarajiwa kuongozana na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohammed Mchengerwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro pamoja na viongozi wengine mbalimbali wa kitaifa.**

"Maandalizi yote yamefikia hatua nzuri huku tukisubiri kumpokea Waziri Mkuu katika maadhimisho haya ya miaka 20," ilisema taarifa ya waandaaji.

Kiongozi huyo wa nchi anatarajiwa kushiriki katika mbio za kilomita tano ambazo zinadhaminiwa na Grand Malt kabla ya kuendelea na shughuli za sherehe ya miaka 20 zitakazofanyika kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi (MoCU).

Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Irene Mutiganzi, ambaye bia yake ni mdhamini mkuu wa Kilimanjaro marathon, alisema wanayo furaha kuungana na Waziri Mkuu katika maadhimisho ya miaka 20 kwani inaonyesha uzito wa shughuli hii.

"Hii inaonyesha ni jinsi gani Kilimanjaro Marathon imekuwa mwaka hadi mwaka na hata kuwavutia viongozi wa kitaifa," Mutiganzi alisema huku akitoa wito kwa washiriki kuendelea kujifua vizuri na kuhudhuria kwa wingi.

Wadhamini wakuu wa mbio za Kilimanjaro Marathon 2022 ni Kilimanjaro Premium Lager wakati Tigo inadhamini mbio za kilomita 21 na wadhamini wa meza za maji ni Absa Tanzania, Unilever Tanzania, TPC Sugar, Simba Cement na maji ya Kilimanjaro Water huku wasambazaji rasmi ni Garda-World Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel, CMC Automobiles na Surveyed Plots Company Ltd (SPC) na Bodi ya Utalii (TTB).

Mbio za Kilimanjaro Marathon zimeandaliwa na Taasisi ya Kilimanjaro Company Limited na kuratibiwa na wadau wa hapa nchini, Kampuni ya Executive Solutions.




## Mwalimu Simiyu ashinda Jackpot

Na Mwandishi Wetu

MKAZI wa Lamadi, Wilaya ya Busega mkoani Simiyu, Shabani Forogo, ameshinda Sh. milioni 16, katika Jackpot Bonus ya Sportpesa iliyochezwa mwishoni mwa wiki iliyoisha, baada ya kupatia kwa usahihi mechi 12.

Akizungumza baada ya makabidhiano ya mfano wa hundi katika ofisi za Sportpesa jijini Dar es Salaam, Forogo alisema alianza kucheza na Sportpesa mwaka jana, baada ya kuona marafiki zake wakishinda.

Forogo ambaye ni mwalimu wa Shule ya Msingi Muungano, alisema alivutiwa na Sportpesa baada ya kuona na kusikia matangazo kuhusiana na Sportpesa kupitia mitandao ya kijamii na kwa watu wa karibu.

"Ujue nina rafiki zangu ambao wote walikuwa wanacheza Sportpesa na nilikuwa nawaona wanacheza na pia wengine walikuwa wanashinda na kunishauri nicheze, hivyo walinitamanisha na mimi kujaribu bahati yangu, kuna mmoja alishinda ya timu 10 na kushinda jackpot bonus, hivyo ilipelekea mimi kupata mshawasho mkubwa kupambania Jackpot,'' alisema mshindi huyo.

Kwa upande wa Sportpesa Meneja Uhusiano, Sabrina Msuya, alimpongeza sana Shabani kwa ushindi wake.

"Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Shabani kwa kubashiri mechi 12 kwa usahihi kati 13".

"Hii ni ishara ya kwamba kushinda hii Jackpot inawezekana, kumbuka kuwa unaweza kuweka mkeka zaidi ya mmoja au kubashiri kwa combination," alimaliza.

Kwa wiki hii kiwango cha Jackpot ni Sh. milioni 940.8.

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/02/22 | 18:00 | Zaragoza vs Las Palmas UD | 2.80 | 3.19 | 2.44 |
| 02. 19/02/22 | 18:00 | Luton Town vs West Bromwich | 2.74 | 3.03 | 2.59 |
| 03. 19/02/22 | 19:00 | Lens vs Lyon | 2.75 | 3.40 | 2.46 |
| 04. 19/02/22 | 20:30 | Oostende vs Standard Liege | 2.55 | 3.34 | 2.60 |
| 05. 19/02/22 | 20:30 | Cadiz CF vs Getafe | 3.05 | 2.95 | 2.55 |
| 06. 19/02/22 | 21:00 | Niort vs AJ Auxerre | 2.70 | 2.95 | 2.70 |
| 07. 20/02/22 | 13:30 | Gaziantep BB vs Adana Demirspor | 2.58 | 3.27 | 2.63 |
| 08. 20/02/22 | 14:15 | PEC Zwolle vs Groningen | 2.38 | 3.24 | 2.85 |
| 09. 20/02/22 | 14:30 | Fiorentina vs Atalanta | 2.85 | 3.45 | 2.38 |
| 10. 20/02/22 | 16:00 | Fatih Karagumruk vs Sivasspor | 2.60 | 3.19 | 2.65 |
| 11. 20/02/22 | 17:00 | Venezia vs Genoa | 2.55 | 3.21 | 2.80 |
| 12. 20/02/22 | 18:30 | Maritimo vs Famalicao | 2.39 | 3.26 | 2.86 |
| 13. 20/02/22 | 19:30 | Wolverhampton vs Leicester | 2.42 | 3.15 | 3.05 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 18/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 4988 | Ahi Nazareth vs Hapoel Rishon Lezion | 2.31 | 3.02 | 3.26 |
| 16:00 | 5358 | Ironi Hasharon vs Beitar Tel Aviv Ramla | 2.23 | 2.93 | 3.57 |
| 16:00 | 5426 | Hapoel Acre vs Hapoel Ramat Gan | 2.46 | 2.96 | 3.06 |
| 17:00 | 1501 | Teraktor Sazi vs Esteghlal Tehran | 5.80 | 2.81 | 1.75 |
| 19:00 | 4844 | Zlate Moravce vs Dunajska Streda | 3.81 | 3.47 | 1.82 |
| 20:00 | 1928 | HNK Gorica vs Slaven Belupo | 1.88 | 3.37 | 3.70 |
| 20:00 | 2079 | Konyaspor vs Kasimpasa | 1.99 | 3.40 | 3.60 |
| 20:00 | 4895 | Caykur Rizespor vs Basaksehir | 3.80 | 3.45 | 1.91 |
| 20:00 | 5768 | Zaglebie Lubin vs Wisla Plock | 2.50 | 3.12 | 2.64 |
| 20:30 | 1837 | Austria Vienna II vs Floridsdorfer AC | 2.71 | 3.38 | 2.30 |
| 20:30 | 3469 | FC Juniors OO vs Rapid Vienna II | 2.84 | 3.56 | 2.14 |
| 20:30 | 4289 | SV Horn vs Liebherr Gak | 3.03 | 3.65 | 2.02 |
| 21:00 | 1600 | Orleans vs Saint Brieuc | 2.02 | 3.18 | 3.62 |
| 21:00 | 2392 | Sedan vs Le Mans | 2.55 | 2.89 | 2.89 |
| 21:00 | 2755 | Sonderjyske vs Aarhus | 3.20 | 3.25 | 2.20 |
| 21:00 | 4552 | Verl vs Zwickau | 2.06 | 3.54 | 3.19 |
| 21:00 | 4951 | Concarneau vs Cholet | 1.67 | 3.45 | 5.06 |
| 21:00 | 5535 | Viseu vs Leixoes | 2.54 | 3.08 | 2.73 |
| 21:00 | 5600 | Boulogne vs Bastia Borgo | 2.06 | 3.27 | 3.41 |
| 21:00 | 5802 | Sete 34 FC vs Chateauroux | 3.57 | 3.13 | 2.06 |
| 22:00 | 3080 | Fortuna Sittard vs Sparta Rotterdam | 2.71 | 3.20 | 2.51 |
| 22:00 | 3447 | Maastricht vs Jong AZ Alkmaar | 2.84 | 3.38 | 2.29 |
| 22:00 | 3707 | FC Eindhoven vs ADO Den Haag | 2.40 | 3.31 | 2.73 |
| 22:00 | 3987 | Roda Kerkrade vs De Graafschap | 2.35 | 3.32 | 2.78 |
| 22:00 | 4301 | Emmen vs FC Volendam | 2.01 | 3.47 | 3.33 |
| 22:00 | 4415 | Dordrecht vs FC Oss | 3.18 | 3.57 | 2.04 |
| 22:00 | 5171 | Telstar vs NAC Breda | 3.07 | 3.41 | 2.14 |
| 22:00 | 5375 | Helmond Sport vs VVV Venlo | 3.02 | 3.36 | 2.19 |
| 22:00 | 5734 | Den Bosch vs Jong PSV | 3.03 | 3.37 | 2.18 |
| 22:25 | 2219 | Blau Weiss Linz vs Vorwarts Steyr | 1.25 | 5.59 | 8.10 |
| 22:30 | 4173 | Mainz vs Bayer Leverkusen | 3.03 | 3.68 | 2.16 |
| 22:30 | 5415 | Stal Mielec vs Pogon Szczecin | 4.64 | 3.33 | 1.71 |
| 22:45 | 1182 | Athlone Town vs Waterford Utd | 4.43 | 3.70 | 1.66 |
| 22:45 | 1191 | Wexford Youths vs Treaty United | 2.70 | 3.22 | 2.39 |
| 22:45 | 1565 | Dunfermline vs Partick Thisle | 2.56 | 3.15 | 2.66 |
| 22:45 | 1651 | Southend vs Grimsby | 2.36 | 3.17 | 2.88 |
| 22:45 | 2171 | Bray Wanderers vs Cork City | 1.99 | 3.32 | 3.37 |
| 22:45 | 2335 | Bournemouth vs Nottingham | 1.80 | 3.53 | 4.12 |
| 22:45 | 3623 | Larne vs Glentoran Belfast | 2.50 | 3.26 | 2.54 |
| 22:45 | 3670 | KAA Gent vs RFC Seraing | 1.29 | 5.14 | 9.29 |
| 22:45 | 4543 | Shelbourne vs St Patricks | 3.27 | 3.08 | 2.13 |
| 22:45 | 5442 | Rotherham vs Wigan | 1.98 | 3.34 | 3.64 |
| 22:45 | 5541 | Dundalk FC vs Derry City | 2.11 | 3.22 | 3.17 |
| 22:45 | 5710 | Juventus vs Torino | 1.66 | 3.71 | 5.33 |
| 23:00 | 3131 | Elche vs Rayo Vallecano | 2.78 | 2.98 | 2.73 |
| 23:00 | 3784 | FC Cartagena vs Valladolid | 2.99 | 3.28 | 2.27 |
| 23:00 | 4014 | Lille vs Metz | 1.41 | 4.49 | 7.59 |
| 23:00 | 5827 | Shamrock Rovers vs UCD Dublin | 1.24 | 4.97 | 10.52 |
| 23:00 | 5896 | Finn Harps vs Drogheda Utd | 2.33 | 2.98 | 2.98 |
| 23:15 | 1899 | Boavista vs Benfica | 6.70 | 4.73 | 1.40 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Ijumaa Februari 18, 2022
Nipashe



Usajili Spurs wamkera Conte UKURASA 21




Mshambuliaji wa Simba, John Bocco (katikati), akiruka kufunga bao la kwanza huku kipa wa Ruvu Shooting, Mohamed Makaka, akishindwa kuokoa shambulio hilo katika mechi ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda mabao 7-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba gari limewaka

## ●●● Yatamba sasa molari imerejea na itaendeleza dozi kwa kila...

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Simba kikitarajia kupaa kuelekea Niger leo jioni, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pablo Franco, amesema ushindi walioupata katika michezo miwili mfululizo iliyopita imerudisha molari kwa wachezaji wake na kuleta matarajio ya kufanya vizuri kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Gendarmarie itakayochezwa keshokutwa.

**Jumapili iliyopita Simba ilipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Asec Mimosas katika mechi ya kwanza ya Kundi D kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na juzi iliwapa kichapo cha bila huruma cha magoli 7-0, Ruvu Shooting kwenye mashindano ya Kombe la FA.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Pablo alisema wachezaji wake walionyesha mchezo mzuri na kiwango bora dhidi ya Ruvu Shooting kwa kutumia vyema nafasi walizopata na kupelekea kuondoka na ushindi mnono.

Pablo alisema bao la mapema walilopata kabla ya kuongeza mengine manne na kwenda mapumziko wakiwa mbele kwa magoli 5-0 lilisababisha wachezaji wake kucheza kwa kujiamini.

"Ushindi wa leo (juzi), umerejesha morali kwa wachezaji, matumaini ya kuendelea kushinda ni makubwa kwa kuwa timu imeanza kuzoeana, tulicheza muda mrefu, tulikuwa na nafasi ya kupata mabao mengi zaidi kipindi cha kwanza," alisema na kuongeza; Ushindi huu umeongeza hali ya kujiamini kwa wachezaji na utulivu umeongezeka, naamini tutaendelea kupata ushindi mnono kwa mechi zetu zijazo," alisema Pablo.

Kuhusu kiungo, Clatous Chama kutocheza michuano ya kimataifa, alimtaja nyota huyo atakuwa miongoni mwa wachezaji watakaosafari kwenda Niger na baadaye Morocco kwa majukumu maalumu huku wakipanga kuweka kambi ya siku chache kabla ya kuunganisha kuelekea Morocco kuvaana na RS Berkane.

"Chama atakuwa katika msafara kwa sababu aliwahi kucheza ndani ya klabu hicho (RS Berkane), anafahamu mazingira pamoja na wapinzani wetu, itakuwa rahisi kwa sababu tuna mchezaji ambaye ametoka ndani ya klabu hiyo na kufahamu mambo mengi kuhusu wapinzani wetu," Pablo alisema.

Aliwataja wachezaji watakaokosekana katika mchezo wa Jumapili ni pamoja na Hassan Dilunga, Dennis Kibu, Chris Mugalu na Taddeo Lwanga ambao bado wako katika uangalizi wa daktari.

"Kuhusu Sadio Kanoute na Pape Ousmane Sakho wako fiti na tuliwapumzisha kwa ajili ya mchezo ujao dhidi ya US Gendarmarie ambao watakuwapo katika mipango ya kikosi chake," alisema Pablo.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema sasa gari limeweka na yoyote atakayekuwa mbele yao atakutana na maafa makubwa iwe katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara au Kombe la FA.

Ahmed alisema baada ya kipindi kigumu walichopita sasa wamerejea katika makali yao na matarajio waliyokuwa nayo ni kuendeleza vichapo kama ilivyotokea kwa Ruvu Shooting.

"Hizi mechi mbili tulizocheza na kushinda bao 10 ni salamu tosha kwa wapinzani wetu, maana katika michuano ya ASFC, tumecheza mechi tatu na kushinda bao 14, tulimfumga bao 1-0 JKT Tanzania, halafu tukamfunga Dar City 6-0 na leo (juzi), Ruvu Shooting amepigwa wiki (7-0)," alisema meneja huyo na kuongeza.

"Lakini Simba ni timu pekee ambayo haijafungwa katika michuano hii na ushindi huu wa leo dhidi ya Ruvu Shooting ni ushindi wangu wa kwanza wa mabao mengi tangu nimeanza kazi Simba, jambo la kujivunia," alisema Ally.

# Yanga yaishtukia Mtibwa Sugar FC

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HUKU Mtibwa Sugar ikisisitiza mechi yao itachezwa kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro keshokutwa, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, ametamba ameendelea kukisuka kikosi chake ili kiwe imara zaidi kwa ajili ya kuondoka na pointi tatu katika mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Nabi aliliambia gazeti hili licha ya kuwakosa baadhi ya nyota wake, hana hofu kwa sababu ameshakiandaa vizuri kikosi chake kuhakikisha kinaendelea pale walipoishia kutafuta pointi tatu.

Kocha huyo alisema hana wasiwasi juu ya uwanja kwa sababu amewapa wachezaji wake mbinu mpya za kiufundi kwa ajili ya mchezo huo kwa kuzingatia mazingira halisi ya uwanja watakaochezea.

"Tunatambua hali halisi ya viwanja tunavyoenda kucheza mechi za ugenini kuwa si bora kama cha Benjamin Mkapa, uwanja isiwe sababu tukiwa hapa tulipoteza pointi mbili dhidi ya Mbeya City, lakini tulifanikiwa kupata pointi tatu ugenini na viwanja sio vizuri ," alisema Nabi.

Alisema kazi kubwa aliyonayo ni kuendelea kukiimarisha kikosi chake na kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika michezo iliyopita ikiwa kuwataka safu ya ushambuliaji iongeze umakini na utulivu.

Aliongeza watashuka uwanjani kuivaa Mtibwa Sugar kwa tahadhari kwa sababu wanafahamu wapinzani wao hawatabweteka.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kwao kila mechi ni muhimu kwa sababu wanataka kumalizika mechi zote za mzunguko wa kwanza bila kupoteza na wamejiandaa kikamilifu kufikia malengo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >